

**UNOMINISHAJI NA UTENZISHAJI WA MANENO YA KISWAHILI
KATIKA REJISTA ZA MAGAZETINI**

KHADIJA ABUBAKAR HUSSEIN

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI
(M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA KATIKA
IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI**

2023

UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo *Unominishaji na Utenzishaji wa Maneno ya Kiswahili katika Rejista za Magazetini* na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya uzamili katika Chuo kuu Huria cha Tanzania.

.....

Dkt. Zelda Elisifa

(Supervisor)

Tarehe.....

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, ama iwe kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, bila kibali cha mwandishi au idhini ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, **Khadija Abubakar Hussein**, nathibitisha kuwa kazi hii ni yangu na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine.

.....
Khadija Abubakar Hussein

Tarehe

TABARUKU

Kwako, baba mpendwa,

Abubakar Hussein Fadhili naitabaruku kazi hii kwako iwe mwanga wa matumaini
huko mbele za haki ulipo.

SHUKURANI

Kwanza kabisa napenda kutoa shukurani za dhati Kwa Allah (sw), Muumba wa mbingu na ardhi kwa kunijaalia uhai, uzima na kunipa uwezo wa kuandika na kukamilisha kazi hii ya utafiti .

Pili, shukurani zangu za pekee ziende kwa msimamizi wangu, Dkt Zelda Elisifa, kwa kukubali kusimamia kazi yangu hii kwa bidii na moyo wa upendo, Mwenyezi Mungu amzidishie moyo wa imani na ampe nguvu aweze kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Tatu, napenda kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine kukamilika kwa kazi yangu hii akiwemo Mwalimu Ramadhan Haji Khamis na watendaji wote wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA).

Nne, shukrani zangu za dhati nazitoa kwa mume wangu mpenzi Bw Masoud Omar Hassan kwa kunipa fursa ya kuendelea na masomo yangu haya bila ya kujali usumbufu ambao alikuwa akipata katika kipindi chote cha masomo. Allah atuzidishie mapenzi. Sitosahau kuwashukuru wazazi wangu wapendwa baba yangu Abubakar Hussein Fadhil na mama yangu Asya Said Mkarafuu ambao walinilea na kunisomesha kwa hakika walipoteza mali zao nyingi kwa ajili yangu hadi kufikia kiwango hiki.

Mwisho, nitakuwa mpungufu wa fadhila kwa kukosa kumshukuru mkuu wangu wa shule Bw Makame Juma Makame kwa kutoninyima ruhusa pale ilipojiri kuomba ruhusa ili niweze kuendeleza kazi yangu pamoja na ndugu Said Abubakar Hussein na Abdulfatah Abubakar Hussein kwa kuniongoza na kunisaidia kufanikisha kazi hii. Nyote nawambieni ahsanteni sana.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza miundo ya unominishaji na utenzishaji katika gazeti la *Zanzibar leo*. Utafiti huu uliongozwa na malengo mawili ambayo ni kubainisha maneno yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa katika lugha ya Kiswahili na pili, kufafanua miundo ya maneno iliyotumika katika kunominisha na kutenzisha katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Aidha, nadharia ya mofolojia, Leksika na usarufishaji zilitumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Data za utafiti huu zilikusanywa kupitia mbinu ya usomaji wa nyaraka za gazeti la *Zanzibar leo*. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni orodha ya maneno yaliyochukuliwa na kuchunguzwa katika gazeti la *Zanzibar leo*. Jumla ya maneno ishirini na tano (25) yalibainika kuwa yamenominishwa ambayo ni sawa na asilimia 47 za maneno yote yaliyochunguzwa. Vilevile, maneno ishirini na sita (26) yalibainika kutenzishwa katika gazeti hilo, ambayo ni sawa na asilimia 53 ya maneno yote. Matokeo ya utafiti huu yameonesha miundo na viwango mbalimbali vya unominishaji na utenzishaji vimejitokeza katika gazeti la *Zanzibar leo*. Matokeo haya, yanathibitisha kuwa uandishi wa magazeti hutumia mbinu za usarufi katika kunominisha na kutenzisha. Ingawa wengi wao hawatumii miundo hiyo kwa taaluma bali hutumia kama ni mazoea katika matumizi ya lugha ya uandishi wa habari. Utafiti huu unapendekeza kufanyika tafiti zaidi kuhusu sarufi ya lugha hasa katika uandishi wa magazeti katika maeneo ya uchomozi wa virai namuundo wa uchanganuzi lugha na athari zake katika magazeti ya udaku, na ushikamani wa matini katika habari.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO.....	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA MAJEDWELI	xii
ORODHA YA VIELELEZO	xiii
ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA	xiv
SURA YA KWANZA: 1.0 UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.2 Tamko la Utafiti	5
1.3 Malengo ya Utafiti	6
1.3.1 Lengo Kuu	6
1.3.2 Malengo Mahususi.....	6
1.3.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.4 Umuhimu wa Utafiti	7
1.5 Mipaka ya Utafiti	7
1.6 Vikwazo vya Utafiti	8
1.7 Muhtasari wa Sura	8

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA

	KINADHARIA	9
2.1	Utangulizi.....	9
2.2	Dhana ya Rejista katika Magazeti.....	9
2.3	Maandiko Kuhusu Uandishi wa Magazetini Duniani	12
2.4	Maandiko Kuhusu Uandishi wa Magazetini Barani Afrika.....	14
2.5	Miundo ya Uandishi wa Magazetini Nchini Tanzania.....	18
2.6	Mkabala wa Kinadharia	21
2.6.1	Nadharia ya Mofolojia Leksika.....	21
2.6.2	Mapungufu ya Nadharia ya Mofolojia Leksika	22
2.5.3	Nadharia ya Usarufishaji.....	22
2.7	Kazi Tangulizi zilizotumia Nadharia ya Mofolojia leksika na Usarufishaji..	24
2.8	Pengo la utafiti	26
2.9	Muhtasari wa Sura	26
	SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	27
3.0	Utangulizi.....	27
3.1	Eneo la Utafiti	27
3.2	Usampulishaji wa Watafitiwa	27
3.3	Mbinu za Kukusanyia Data.....	28
3.4	Mbinu za Uchanganuzi na Uchambuzi wa Data.....	28
3.4.1	Uchanganuzi wa Data	28
3.5	Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti.....	29
3.6	Muhtasari wa Sura	29

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA	30
4.1 Utangulizi.....	30
4.2 Maneno Yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa Katika Lugha ya Kiswahili	30
4.3 Miundo Iliyotumika katika Unominishaji wa Maneno	33
4.3.1 Muundo wa Kiambishi awali {mu, m} + shina- KT+ kiambishi tamati {ji}..	34
4.3.2 Muundo wa Unominishaji unaotokea kwa vijenzi vya Mz+o (kt)	37
4. 3.3 Muundo wa Unominishaji wa kijenzi U+Mz+ zi	39
4.3.4 Muundo wa Unominishaji kwa maneno yanayotokana na sifa	40
4.3.5 Upachikaji wa kiambishi {o} tamati kwenye vitenzi vinavyoishia na kiambishi {-a} tamati.....	43
4.3.6 Maneno yaliyonominishwa kwamuundo wa m + {-i/-li-} + {-o }	44
4.3.7 Kupachika kiambishi {ku} ya unominishi.....	45
4.4 Muundo ya Utenzishaji wa Maneno Kutoka Katika Gazeti la Zanzibar Leo	46
4.4.1 Utenzishaji wa viambishi vya unyambuuji -esh na -ish.....	47
4.4.2 Utenzishaji wa kiambishi {- k- }cha k/utendeka	49
4.4.3 Utenzishaji wa vipashio vya {-isha} kutoka katika nomino	50
4. 4.4 Muundo wa Utenzishaji unaotokana na nomino {sh+i}	51
4.5.5 Muundo wa utenzishaji unaotokana na Vivumishi.....	52
4.4.6 Kiambishi Nyambuo Tenzishi –a SH+kfTsh.....	52
4. 4.7 Utenzishwaji kutoka kategoria kutumia Iza, Ka, a, Ku	54
4.5 Mustasari wa Sura.....	55

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	56
5.1 Utangulizi.....	56
5.2 Muhtasari wa Utafiti	56
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	58
5.4 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika Kwenye Utafiti.....	58
5.5 Mchango Mpya wa Utafiti	59
5.6 Hitimisho.....	60
5.7 Mapendekezo ya Utafiti	60
5.7.1 Mapendekezo kwa waandishi wa magazeti	61
5.7.2 Mapendekezo Kwa Serikali	61
5.7.3 Mapendekezo kwa tafiti za baadaye	61
MAREJELEO	62
kiambatanisho Na. 1.....	69
Kiambatanisho Na 2.....	71
Kiambatanisho Na. 3.....	72

ORODHA YA MAJEDWELI

Jedwali Na. 1:	Maneno yaliyonominishwa	31
Jedwali Na. 2:	Maneno yaliyotenzishwa	32
Jedwali Na. 3:	Orodha ya Miundo Iliyonominishwa.....	33
Jedwali Na. 4:	Miundo ya unominishaji m/mu+sh+ji	36
Jedwali Na. 5:	Unominishaji wa Kutumiamuundo wa Mz+ktz+o	38
Jedwali Na. 6:	Maneno yaliyonominishwa kwa kutumiamuundo U+Sn+KTMKNz	40
Jedwali Na.7	Muundo inayofuata masharti zuizi	41
Jedwali Na. 8:	Mifano inayonominishwa kwamuundo wa Mz+Sh+a.....	43
Jedwali Na. 9:	Maneno yaliyonominishwa kwamuundo wa m + {-i/-li-} + {-o}.....	44
Jedwali Na 10 :	Maneno Yaliyonominishwa Kwamuundo wa {Mzizi+} + {-e-} + {-o}	45
Jedwali Na. 11:	Mifano ya unominishaji wa kiambishi “ku”.....	46
Jedwali Na. 12:	Orodha ya muundo Iliyotumika Kutenzisha.....	47
Jedwali Na. 13:	Muundo wa utenzishaji wa viambishi vya unyambuaji –esh-.....	48
Jedwali Na .14 :	Mifano ya utenzishaji kwamuundo wa – ish+a	48
Jedwali Na. 15	Muundo wa utenzishaji kwa kufuata MZ/S+KJ+KKS.....	49
Jedwali Na. 16:	Muundo wa utenzishaji kwa kufuata Mz+ish+kt	50
Jedwali Na.17:	Muundo wa utenzishaji kwa kufuata Sh+Ir.....	51
Jedwali Na.18:	Muundo wa utenzishaji unaotokana na Vivumishi	52
Jedwali Na. 19:	Miundo ya utezishaji kwa kutokea kategori tofauti	53
Jedwali Na. 20:	Miundo ya utezishaji kwa kutumia Iza, Ka, a, Ku	54

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na.1: Mfano wa Unominishaji	35
Kielelezo Na.2: Mfano wa unominishaji wa ‘Taratibu’	42

ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA

BAKIZA:	Baraza La Kiswahili La Zanzibar
Ir	irabu
KAK:	kiambisi awali kinominishi
KJ:	kiambishi kijenzi
KK:	kiambishi cha kauli
KN:	Kishazi nomino/ kikundi nomino
KTM:	Kiambishi Tamati Maana
KTMKN:	Kiambishi Tamati Maana Kinominishi
MZ:	Mzizi wa neno
SH	shina la neno

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Gazeti ni chapisho la mara kwa mara lenye habari iliyoandikwa juu jambo la ghafla na matukio yanayokwenda na wakati Magazeti yanaweza kuwa na nyanja anuwai kama siasa, biashara, michezo, sanaa na mara nyingi hujumuisha vifaa kama safu za maoni, utabiri wa hali ya hewa, ukaguzi wa huduma za mitaa, mazishi, matangazo ya kuzaliwa, maneno mafupi, vichekesho, safu za ushauri na wahariri

Taaluma ya uchanganuzi wa vijenzi vya maneno imewashughulisha wataalamu mbalimbali kwa muda mrefu. Katika miaka ya 1920 hadi 1960, wanamuundo kama vile Ferdinand de Saussure, Edward Sapir, Benjamin Whorf, Leonard Bloomfield walishughulikia sana muundo wa maneno hususani katika kiwango cha Mofolojia na walisisitiza kuwa sharti kila kiwango cha lugha kijitegemee. Kwa mantiki hiyo viwango mbalimbali vinavyojitegemea vinaweza kutazamwa katika uandishi wa gazetini. Na ndio maana miundo ya unominishaji na utenzishaji ikiwa ni jambo linaloweza kutazamwa.

Mgullu (2012) ameifafanua dhana ya unominishaji kama isitilahi inayotumika kuelezea utaratibu wa kuunda nomino kutokana na maneno mengine ambayo si nomino. Katika maelezo yake anaendelea kufafanua kwa kusema nomino nyingine za Kiswahili huwa na mofu ambazo huwakilisha mofimu ya unominishaji. Vile vile, Malangwa (2011) amefafanua dhana ya utenzishaji kwa kusema, utenzishaji ni isitilahi yenye maana ya mchakato wa ki Mofolojia wa uundaji wa vitenzi kutokana na aina zingine za maneno zilizo tofauti na kitenzi.

Massamba (2004) anadai kuwa vitenzi yakinifu ni vile vyenye kutoa taarifa au maelezo na ambavyo havihusu swali wala ukanushi.muundo huu hufanywa kwa kutumia mchakato wa ki Mofolojia ujulikanao kama uambikaji/ uambishaji. Kwa mujibu wa maelezo hayo tunaweza kubaini kuwa mchakato wa kutenzisha unaweza kujitokeza kwa miundo tofauti ikiwemo uambishaji au unyambuaji wa maneno.

Waititu na wezake (2004) wanasema kuna vitenzi vya asili ya kibantu na vitenzi vya kigeni. Vitenzi vingi vya asili ya kibantu vina uwezo wa kuchukua viambishi vyenye maana mbalimbali za kisarufi. Anasisitiza kuwa vitenzi vinaweza kunyambuliwa na kuwa kategoria nyingine ya neno kutegemeana na viambishi vilivyopachikwa katika maneno hayo. Maelezo haya hayajaonesha ni kwa kiasi gani vitenzi vinavyopatikana kutoka kategoria nyingine bali yameeleza kuwa vitenzi vinaweza kuhama na kwenda kategoria nyingine. Maelezo hayo yametusaia sana maana yanatoa mwanga wa kuona kuwa maneno mengi ya lugha ya Kiswahili yana uwezo wa kwenda na kubadilika katika kategoria kadhaa za maneno ambapo utafiti huu umeangalia kategoria hizo kwa kuteua nomino na vitenzi vilivyotoka katika kategoria nyingine ya maneno.

Katika kuangalia ubainishaji, Kihore na wenzie (2003) wanathibitisha kuwa kuna uwezekano wa kuzalisha vitenzi kutokana na kategoria nyingine za maneno na wanabainisha mfano mmoja ambao ni kivumishi chafu kuwa kitenzi chafua. Aidha, Kiango (2000) anajadili vinyambuo vya vitenzi vinavyobadili kategoria ya neno katika kipengele cha uundaji wa vitenzi vya mnyambuliko kutokana na kategoria nyingine za maneno. Pia,anabainisha namna ya kuviingiza vitenzi vinavyoundwa na kategoria nyingine za maneno katika kamusi. Anabainisha viambishi nyambuo

tenzishi -esh-, -ish-, -sh- vya utendesha na -ek-, -ik-, -k- vya utendeka kwa data ya maneno yanayodhihirisha dhana ya utenzishaji kupitia unyambulishaji wa utendesha kutoka vivumishi kuwa vitenzi kama ifuatavyo:

- i. bora = boresha
- ii. duni = dunisha
- iii. fupi = fupisha
- iv. zee = zeesha
- v. safi = safisha
- vi. laini = lainisha

Vilevile, data ya pili ya utendeka inayobainishwa na Kiango hapa chini ni ya kategoria ya kivumishi kuunda kategoria ya kitenzi. Tazama data ifuatayo:

- i. -zee = zeeka
- ii. -laini = lainika
- iii. -chafu = chafuka
- iv. -pevu = pevuka
- v. -erevu = erevuka
- vi. -refu = refuka

Maelezo hayo yanaonesha mwelekeo unaojitokeza katika uandishi wa magazetini. Hivyo, data hizi zimeusaidia mno utafiti huu kwa kubaini namna kiambishi “sha” na “ka” kinavyoibadilisha kategoria ya neno kutoka kivumishi kuja kitenzi au kielezi kwenda kitenzi.

Kirichia (2012) amefafanua muundo wa lugha na sajili zake katika gazeti la *Taifa Leo* kwa kusema kwamba lugha ya magazetini hufuata muundo tofauti na maandishi

ya kawaidau kwa vile baadhi ya kauli hazifuati sheria za lugha sanifu. Quarshie (2013) alibaini kuwa asilimia sitini ya magazeti yanayoandika kwa Kiswahili hutumia muundo wa kuchanganya lugha baina ya Kiswahili na Kingereza.

Gupta (2007) anasema uteuzi wa maneno katika magazeti ya biashara ni jambo la msingi na linalopendeza mno. Katika makala yake anaonesha kumekuwa na wimbi kubwa la uchanganyaji wa lugha kama muundo mpya unaotokana na athari ya utandawazi.

Kwa ujumla, maelezo haya yanathibitisha uwepo wa miundo tofauti ya uandishi wa magazeti; yapo yanayoonesha muundo wa kudondosha silabi na baadhi yao wametazama uhariri wa maandishi, na wengine wamefafanua kwa ujumla kuwa kwenye magazeti kuna miundo inayojitofautisha baina ya aina moja ya gazeti na nyingine. Pia, walitathmini namna magazeti yanavyochanganya lugha. Hata hivyo, tafiti hazijatazama kuhusu miundo ya utenzishaji na unominishaji wa maneno yanayojitokeza katika magazeti kutokana na kuwa malengo ya tafiti zao yakulenga upande huu wa unominishaji na utenzishaji. Hata hivyo, tafiti zao zimejiegemeza katika maeneo matatu. Mosi, kuangalia udondoshaji, kuchanganya lugha na haionekani kuwa sarufi inaweza kutumika katika taaluma ya uandikaji wa magazeti, Pia, kwa kuwa tafiti zinaonyesha miundo inatofautiana baina ya gazeti moja na lingine, utafiti huu ulinuia kutazama kwa undani miundo ya unominishaji na utenzishaji wa maneno katika rejista za magazetini hususan katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

1.2 Tamko la Utafiti

Msukumo wa utafiti huu ni kuchunguza miundo itumikayo katika uandishi wa magazeti hususani kupitia unominishaji na utenzishaji kwani kumekuwa na tatizo kubwa linalotokana na lawama za viongozi wa kisiasa kuwa waandishi wa gazeti la *Zanzibar Leo* hawafuati kanuni za lugha katika uandishi wa habari zao¹. Hata hivyo baadhi ya watafiti kama vile Kombo (2006) na Kezilahabi (1983) wamefafanua miundo ya ushairi wa magazetini kwa kuchunguza sifa, maadili na miundo ya uandishi katika magezeti mbalimbali. Aidha wameeleza kwa kiasi gani miundo ya mashairi ya magazetini yanabeba nyanja mbali mbali za isimu kama vile udondoshaji wa maneno.

Pia, Mwansoko (1991) amefafanua miundo inayotumika katika magazeti huku akisisitiza miundo ya vichwa vya habari inavyotumia uchopekaji wa rejista za mazungumzo ya mitaani katika maandishi rasmi. Vile vile, Amadi (2010) alichunguza uteuzi wa maneno katika magazeti ya Nigeria yenye habari za kisiasa kwa kuangalia muundo wa vichwa vya habari. Katika utafiti huo alibaini matumizi makubwa ya udondoshaji wa mofimu ya wakati.²

Kwa ujumla, tafiti zilizotangulia zimetafiti miundo ya uandishi na kubaini uchopekaji au udondoshaji wa mofimu, muundo ya uandishi wa vichwa vya habari, lugha inayotumika katika matangazo ya biashara na lugha ya ushairi wa magazeti. Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanyika kuchunguza miundo ya unominishaji na

¹ Maelezo ya Rais mstaafu Dkt. Ali Muhammed Shein katika kongamano la pili la Kiswahili la kimataifa lililofanyika Zanzibar tarehe 20/12/2018 yalionya gazeti la Zanzibar leo kwa kutumia miundo isiyoridhisha katika uandishi wa habari kwenye gazeti hilo.

² Amadi, F. (2010). *The Role of Nominalization in Newspaper Coverage of the 2005 National Political Reform Conference in Nigeria*.

utenzishaji katika gazeti la *Zanzibar leo*. Hivyo utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo la utafiti.

1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu hizo ni lengo kuu na malengo mahususi kama yanavyobainishwa hapa chini.

1.3.1 Lengo Kuu

Kutathmini unominishaji na utenzishaji wa maneno ya Kiswahili katika rejista za magazeti.

Lengo hili liliongozwa na malengo mahususi mawili kama yalivyoorodheshwa katika kipengele cha 1.3.2.

1.3.2 Malengo Mahususi

- i. Kubaini maneno yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa katika lugha ya Kiswahili katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo*
- ii. Kufafanua miundo ya maneno yaliyotenzishwa na yaliyonominishwa katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

1.3.3 Maswali ya Utafiti

- i. Ni maneno yepi yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa katika lugha ya Kiswahili katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo* ?

- ii. Miundo ipi ya maneno yaliyotenzishwa na yaliyonominishwa katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo*?

1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaleta tija kadha kwa jamii. Miongoni mwa tija hizo ni:

Mosi, utafiti utasaidia njia mbadala ya uzalishaji wa maneno katika vyombo vya habari na kuongeza taaluma ya miundo ya uundaji wa maneno na kanuni zinazokubalika katika lugha ya Kiswahili katika kuunda maneno.

Pili, utafiti huu unaleta mwanga kwa tafiti zinazotazama miundo mbalimbali ya utenzishaji na unominishaji katika magazeti.

Tatu, kwa vile utafiti huu unachunguza tawi la isimu katika utokeaji wa kategoria za maneno kwamuundo wa unominishaji na utenzishaji, utasaidia jamii kuwa na uelewa mpana katika taaluma ya isimu hasa kwenye uga wa uundaji wa maneno.

1.5 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza miundo ya unominishaji na utenzishaji wa maneno yanayoandikwa katika *Gazeti la Zanzibar Leo*. Katika kuchunguza vipengele hivi mtafiti aliangalia namna miundo hiyo inavyodhihirika katika habari za michezo pamoja na siasa hapo taaluma ya kimofonolojia na sintaksia zimesaidia kubaini maumbo ya maneno yanavyobadilika kutoka kategoria moja kwenda kitenzi au nomino. Kategoria nyingine za maneno kama vielezi, vivumishi na viwakilishi hazikuhusishwa katika utafiti huu.

1.6 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti huu ulikabiliwa na ugumu wa upatikanaji wa rejea za Kiswahili zinazohusu uandishi wa magazeti. Jitihada ilifanyika katika kupakua vitabu mbalimbali vya mtandaoni na kuvisoma ingawa vilikuwa ni vya Kiingereza. Pia, uhaba wa fedha za kununua magazeti ya Zanzibar leo kwa mwaka mzima. Jambo hili lilitatuliwa kwa kuomba magazeti katika shirika la magazeti ya serikali pamoja na kupakuwa baadhi ya magazeti katika mitandao ya kijamii.

1.7 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii kumefafanuliwa kwa uwazi usuli wa tatizo, tamko la tatizo, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na mipaka ya utafiti na kuhitimisha na vikwazo vya utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sehemu hii imepitia kwa undani mapitio ya maandiko yanayohusiana na rejista za magazetini duniani, Afrika, Tanzania na hatimaye Zanzibar. Maandiko haya ni yale yanayohusiana kwa ukaribu na malengo ya utafiti huu. Nadharia zilizoongoza utafiti huu pamoja na pengo la utafiti vitaangaziwa kwa undani.

2.2 Dhana ya Rejista katika Magazeti

Yule (2010) anasema rejista ni njia ya mazungumzo yanayotawaliwa na eneo maalumu (kama vile kanisani), kazi maalumu (kama vile urubani), mada maalumu (kama vile taaluma ya lugha) watu maalumu (kama vile wanafunzi). Kwa mujibu wa maelezo ya Yule (keshatajwa) rejista imehusishwa na taaluma maalumu na watu maalumu, hivyo maelezo yake ni muhimu kwa sababu yamesaidia kubaini kuwa rejista inaweza kuchunguza katika taaluma yeyote., ambapo utafiti huu umeteuwa taaluma ya uandishi wa habari katika maandishi yaliyopo katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

Brown (2000) anaona kuwa rejista nimuundo maalumu wa lugha za kijamii au lugha za kimaeneo zinazotumiwa kwa madhumuni mahususi. miundo ya lugha inaweza kutofautiana sana katika utumiaji wa lugha moja na nyingine kutegemeana na mada, wahusika, na hata eneo la mazungumzo. Kwa hivyo inaweza kubishaniwa kuwa rejista wakati mwingine hutumiwa vibaya kama kisawe cha mtindo. Brown (keshatajwa) yanaonesha wazi kuwa rejista inahitaji mada maalumu na taaluma

maalumu. Hivyo basi, utafiti huu umeteua eneo la uandishi wa habari za magazetini ili kuchunguza miundo itumiwayo kunominisha au kutenzisha maneno.

Kabellow (2019) amechunguza jinsi lugha za rejista zinavyoathiri lugha ya kufundishia katika lugha ya Kiingereza kwenye shule za upili nchini Kenya. Makala yake inaangazia hasa jinsi rejista mbalimbali za lugha zinazotumiwa na walimu na wanafunzi katika madarasa ya lugha ya pili ya Kiingereza. Hata kama, makala hii imetazama lugha inavyotumika katika ufundishaji lakini imeonesha kuwa rejista zinaweza kutumiwa katika maeneo tofauti rasmi na zikatoa athari katika eneo hilo. Hivyo, utafiti wetu umeona ipo haja ya kutazama rejista za magazetini katika uga wa unominishaji na utenzishaji wa maneno.

Denutus (2017) amefafanua dhana ya rejista kwa kusema rejista nimuundo maalumu wa lugha unaotegemeana na kazi fulani, muktadha wa mazungumzo, lengo la mazungumzo, na uhusiano wa wanaowasiliana. Rejista hujitokeza katika maeneo tofauti hutegemea na kazi inayofanywa katika maeneo hayo. Kwa mfano, eneo la ufundi, mahakamani, hotelini, matangazo na mazungumzo ya mawaidha au mihadhara hutegemewa kuwa namuundo mbalimbali ya mazungumzo, ambayo baadhi ya wataalamu huziita kuwa ni sajili za maneno.³ Lugha ya Kiswahili inakua, inabadilika na kusambaa kwa kasi. Sehemu kubwa ya mabadiliko hayo huchochewa na maendeleo katika nyanja kama vile sayansi na teknolojia. Mabadiliko hayo huzua haja ya ukuzaji wa lugha ili kuiwezesha kuwasilisha dhana mpya katika maisha ya kila siku (Ohly, 1987). Katika maelezo haya ni dhahiri kuwa ndani ya magazeti zipo

³ Denutus (2017) matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali makala iliyoandikwa katika jarida la mtandaoni, *Blog achieve* la Kenya.

rejista maalumu zinazopaswa kutumika. Rejista ambazo ndizo zinazoweza kuibua miundo mbalimbali ya lugha katika nyanja ya isimu.

King'ei (2000) anasema lugha ya kimagazeti inaweza kuwa ya maelezo, ufimanishaji au ulinganishi, usisitizaji, ukinzani (utatanishi) na kadhalika. Hata hivyo magazeti yanaweza kueleza dhana moja kwa moja (udhahiri), kwamuundo wa maana husishi (km. mkora, mwaminifu, mfisadi, mcha Mungu). Aina ya maana hizi huzingatiamuundo maalumu; yaani kisajili au kirejista. Maelezo katika makala hiyo yanaonesha waziwazi kuwa katika uandishi wa magazeti ipo miundo / sajili au rejista ambazo zinatumiwa na upande wa pili zinaweza kuibua miundo ya kiisimu kama vile kubadili aina moja ya neno kwenda aina nyengine.

King'ei (2000), amewanukuu Crystal na Davy (1969), wanasisitiza kuwa makala katika vyombo vya habari hugubika nyanja tofauti: habari, tahariri, michezo, makala maalum, burudani, uchambuzi, ripoti, mahojiano, maoni, matangazo na nyanja nyinginezo. Nyanja zote hizi huzingatia miundo mbalimbali na pia mbinu tofauti za uteuzi wa lugha. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa vyombo vya habari vinamuundo wake au sajala yake maalum. Ni dhahiri kuwa maelezo hayo yanaakisi moja kwa moja ushahidi wa kuwepo kwa miundo tofauti ya lugha ndani ya magazeti. Jambo ambalo linachochea ari ya kufanya utafiti huu ili kuweza kubaini ni miundo ipi hutumiwa na waandishi katika magazeti yao.

Katika kupitia ufafanuzi wa Kirichia (2012), miundo ya lugha na sajili zake katika gazeti la *Taifa Leo*, lugha ya magazetini hufuatamuundo tofauti na maandishi ya kawaida. Baadhi ya kauli hazifuati sheria za lugha sanifu. Kauli zinginezo zimejaa

taharuki ili kuamsha hamu ya wasomaji. Kwa mfano, katika “Kenya yashinda”, msomaji hubaki kujiuliza, imeshinda nini? Magazeti hunuia kutoa habari ili kuburudisha, kujuza na kuelimisha. Sifa za sajili ya magazeti ni nyingi. Mifano ya sifa hizi ni kama maandishi makubwa na yale madogo na pia wino uliokoza na hafifu. Vichwa vya habari huandikwa kwa herufi kubwa na huwa ni vichwa vifupi vifupi ambavyo vinavutia. Vichwa hivyo vinakuwa utata uliokusudiwa na vinajenga taharuki. Habari zilizoripotiwa hurudiwa ili kusisitiza na kujenga kumbukumbu. Maelezo haya ni muhimu sana kwani yanatoa mwanya wa kuona kwa kiasi gani miundo ya uandishi inayotamalaki katika magazeti.

2.3 Maandiko Kuhusu Uandishi wa Magazetini Duniani

Maandiko kadha yamefafanua kuhusu miundo ya uandishi. miundo ambayo hutofautiana kati ya nchi moja na nyingine, lugha moja na nyingine au lengo la gazeti moja na lengo gazeti jingine.

Hanifa (2008) amefanya utafiti kuhusu upachikaji wa viambishi awali katika vichwa vya habari vya Gazeti la “*Jakarta Post Newspaper* katika gazeti hili mwandishi amejadili namna waandishi wa gazeti hili wanavyotumia aina ya neno na kuligeuza kuwa namna nyingine ya neno kwa kuongeza viambishi awali katika neno. Aidha, ameendelea kusema kuwa aina yoyote ya neno inaweza kufupishwa au kunyambuliwa ili iweze kugeuka kuwa aina nyingine ya neno. Katika utafiti hakutoa mfano wa maneno yaliyotenzishwa au kunominishwa lakini umeweza kutusaidi kujua kuwa katika uandishi wa magazeti upomuundo unaoweza kugeuza maneno kutoka kategoria moja kwenda kategoria nyengine. Utafiti huu uliziba pengo hili kwa

kutazama kwa kiasi gani magazeti yanavyoweza kunominisha na kutenzisha maneno, hususani katika gazeti la *Zanzibar leo*.

Agu (2015) amechunguza miundo ya kisintakisia katika magazeti na kusema kuwa uchaguzi wa maneno huamuliwa kutokana na uwanja wa somo husika. Ili kujaribu kuwasiliana na kundi husika, watu huchukua hatua za kiuielewa kutokana na anuwai ya msamiati uliojitokeza katika kundi hilo la kitaaluma. Maelezo haya yaliufaa sana utafiti huu uliotathamini uandishi katika gazeti la *Zanzibar Leo* kwa kutakidi kuwa uwanja huo unaweza kuwa na misamiati kadha inayotofautiana na kada nyingine.

Kelly-Holmes (2005) alisema kwamba maandishi ya matangazo hutegemea mahusiano ya mwandishi, mtuma tangazo na hadhira. Hivyo uchaguzi wa lugha pia unategemea sana uhusiano huo. Chaguo la lugha lazima ifahamike kwa walengwa pia, uchaguzi wa lugha unaweza kuarifiwa na mhusika wa tangazo. Jambo hili ni la msingi kwani walengwa wa tangazo ni jambo muhimu mno hivyo huandikiwa kwa mujibu wa taaluma zao. Hivyo, hadhi ya taaluma husaidia kuwepo kwa miundo mbalimbali ya lugha jambo ambalo ndio msingi wa utafiti huu katika kubaini miundo mbalimbali ya lugha za magazetini.

Malgwi (2009) alitafiti matumizi ya lugha katika vyombo vya habari na kusesitiza kwamba mtu yeyote anayetumia lugha anajua umuhimu wa msamiati kwa mawasiliano madhubuti. Wazo la kuchagua maneno husisitiza katika uteuzi wa maneno hayo. Kwa hivyo, fani na watendaji tofauti huchagua maneno kulingana na maoni na tabia fulani ya fani zao. Uteuzi huu maalum wa maneno au misemo inahusishwa na shughuli fulani, taaluma au uwanja maalum wa shughuli za

wanadamu; ndio maana utafiti huu ulitafiti uandishi wa habari katika gazeti la *Zanzibar Leo* ili kuona ni kwa kiasi gani katika gazeti hili kunamdhahiriko wa miundo ya uandishi katika utenzishaji na unominishajishaji wa maneno.

2.4 Maandiko Kuhusu Uandishi wa Magazetini Barani Afrika

Sehemu hii inafafanua maandiko kadhaa yanayohusu miundo mbalimbali ya uandishi wa magazetini barani Afrika. Uandishi wa magezeti umefanyiwa tafiti kadhaa na kuandikwa katika maandiko mengi.

Koubali (2007) unaonyesha ni jinsi gani wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya wanavyoteua lugha katika kiwango cha Leksika na sintaksia ili kupitisha ujumbe unaoathiri msomaji kwa njia ambayo mhariri amenuia. Hapa, mtafiti alionesha umuhimu wa uhariri wa magazeti kwamuundo wa kutazama viwango vya msamiati na usahihi wake. Katika utafiti huu mwandishi anasisitiza wahariri kuzipitia taarifa zilizomo magazetini kwa kina ili kuepusha makosa ya kiuakifishaji na kimsamiati. Aidha, mtafiti amefafanua umuhimu wa uhariri kwa waandishi kwa kusisitiza kuwa mwandishi anayehaririwa kazi yake huwa mmahiri kutokana na kujiepushana makosa aliyokosolewa mwanzoni. Maelezo ya hapo juu yalisaidia utafiti huu kubaini kuwa katika taaluma ya uandishi wa magazetini ipo miundo ya upachikaji wa maneno kwa mujibu wa gazeti husika maneno ambayo ndio huzaa vitenzi au nomino. Kwa minajili hiyo kuna sababu ya kupembua na kuchungua gazeti ya *Zanzibar leo* kwa kutazama miundo ya utenzishaji na unominishaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili.

Olumhense (2005) aligundua kuwa uandishi wa magazeti ya Nigeria hayanamuundo bora na umaridadi wa lugha katika uteuzi wa maneno. Katika utafiti wake aligundua

kwa kuwa uandishi wa vichwa vya habari vya magazeti ya Nigeria hayazingatii isimu ya lugha hasa wanapoandika habari za kisiasa.⁴ Utafiti huu umebainisha tatizo la uteuzi wa maneno katika vichwa vya habari vya magazeti, jambo ambalo liliusaidia sana utafiti huu kubaini miundo mbalimbali ya unominishaji na utenzishaji katika harakati za mwandishi kuteua maneno yanayowakilisha kwa usahihi ujumbe unayojitokeza katika uandishi wa magazeti.

Mwaro (2000) kwa upande wake, alitafiti usayansi wa isitilah za kiisimu ya Kiswahili. Katika utafiti wake anaeleza kuwa ipo miundo mingi inayotumika nchini Kenya ya ujinishaji wa maneno/ unominishaji au uundaji wa maneno mapya. Alifafanua kuwa kazi ya uundaji wa maneno au usanifishaji wa lugha nchini Kenya hufanya taasisi zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili. Vyama mbalimbali na taasisi za kielimu ndizo zinazoshughulika na uundaji wa maneno mapya. Amefafanua kwa kusema zipo nadharia kadha zinazotumika katika uundaji wa maneno hayo. Pia, katika kazi hiyo amesisitiza kuwa baadhi ya miundo huwa inakwepa kaida za awali za lugha ili kunusuru utusi, yaani baadhi ya maneno hufichwa ili kuacha kutukana. Utafiti wa Mwaro (keshatajwa) ulitusaidia sana katika utafiti huu kwa kutuonesha kuwa maneno yanaweza kuchakatwa na kupatikana neno jingine hasa pale utengenezaji wa isitlahi unapofanyika. Hivyo, maneno ndiyo yanayotoa isitlahi, hivyo vitenzi na nomino zinaweza kuwa moja wapo ya aina za maneno zilizopita katika mchakato huo. Ikumbukwe kuwa waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kutengeneza istilahi zinazoweza kutumika katika habari zao.

⁴ Makala iliyosomwa katika blog ya mtandaoni <https://mediacareng.org>. blog.

Uchunguzi wa King'ei (2000) kuhusu matatizo ya matumizi ya lugha katika vyombo vya habari vya Kenya, ulibainisha kuwa waandishi wanatarajiwa kutumia lugha sanifu, ila sharti ifahamike kuwa wao wana uhuru wa kiusanii kwa hivyo hawana budi kubuni na kutunga maneno na miundo mipya kila mara. Katika utafiti huu unaonesha kuwa jukumu kubwa la waandishi wa habari ni kuzalisha maneno mapya ambayo yanaweza kuwa aina yoyote ya neno kama nomino au kitenzi. Pia, mwandishi anasisitiza kuwa miundo tofauti ya maneno inaweza kutumika katika magazeti, jambo ambalo ni miongoni mwa malengo ya utafiti huu ya kuchunguza miundo inayotumika katika magazeti.

Kirichia (2012) amefafanua miundo mbalimbali itumikayo katika gazeti la *Taifa leo*, uchambuzi ulionesha kuwa lugha ya magazetini hufuata miundo tofauti ya maandishi. Baadhi ya kauli zilioneshwa kutofuata sheria za lugha sanifu. Baadhi ya kauli zilioneshwa kujaa taharuki ili kuamsha hamu ya wasomaji. Alitoa mfano kwa kusema katika gazeti la *Taifa Leo* kumeandika "Kenya yashinda." Katika mfano huo alisisitiza kuwa uandishi wa magazeti unaweza kudondosha neno au hata sentensi nzima ilimradi wasomaji waweze kuvutiwa na habari hiyo bila kujali kanuni za uandishi. Kwa usahihi ilipaswa kuwa timu ya kenya yashinda. Utafiti huu ulisaidia utafiti wetu kwa kudhihirisha ukweli kuwa kila taaluma inajitegemea katika miundo ya uandishi.

Pia, Kirichia (keshatajwa) anafafanua miundo mbalimbali ya uandishi wa vichwa vya habari na kusema vichwa vya habari huandikwa kwa herufi kubwa na huwa ni vichwa vifupi vifupi ambavyo vinavutia. Vichwa hivyo vina utata na vinajenga taharuki. Habari zilizoripotiwa hurudiwa ili kusisitiza na kujenga kumbukumbu.

Sarufi haizingatiwi kwa kiasi fulani. Msamiati teule hutumiwa na kuna ubunifu wa maneno na ukopaji wa maneno ili kuendeleza mtiririko wa habari. Matumizi ya picha yapo ili kushadidia habari zilizotolewa. Wanahabari hutumia lugha sahili ili kueleweka kwa wanaokusudiwa kupewa habari hiyo. Hapa, tunaona wazi kuwa muundo wa magazetini unatofautiana mno na miundo katika uandishi mwingine cha muhimu katika uandishi ni kuhakikisha kuwa ujumbe umefikia walengwa. Sentensi za magazeti aghalabu huwa fupi fupi ili kuwafanya wasomaji wasichanganye Jambo hilo linatupa ithibati ya kusema kuwa kila maandishi yanaweza kuwa na miundo mbalimbali ya kiuandishi.

Koubali (2007) kwa upande wake alichunguza namna wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* wanavyoteua lugha katika kiwango cha Leksika na sintaksia ili kupitisha ujumbe unaoathiri msomaji kwa njia ambayo mhariri ameiteuwa. Matokeo ya utafiti wake yalifafanua kuwa waandishi wa *Taifa leo* wanajitahidi kuandika kwa usahihi .Hapa mwandishi alijaribu kuonesha umuhimu wa uhariri wa magazeti wamuundo wa kutazama viwango vya msamiati na usahihi wake.

Kulingana na Kombo (2006) kwenye uchunguzi wake wa fani ya mashairi ya UKIMWI katika magazeti ya Kiswahili, mashairi ya magazetini yanatumia takriri kwa kiasi kikubwa kwa kuwa mengi kati yake yanafuata muundo wa kimapokeo wa kutunga mashairi. Matumizi ya takriri katika ushairi na kazi nyingine za fasihi hufanywa kwa ajili ya kutoa msisitizo juu ya jambo ambalo mshairi anataka jamii ilielewe vizuri.

Maelezo hayo yanayakinisha kuwa muundo wa uandishi wa mashairi unatofautiana na muundo wa habari za kibiashara. Hivyo, katika magazeti kunaweza kuwa na miundo tofauti kulingana na muktadha wa habari husika.

2.5 Miundo ya Uandishi wa Magazetini Nchini Tanzania

Katika nchi ya Tanzania, maandiko kadhaa yamefafanua uandishi wa gazetini. Sehemu hii itadondoa baadhi ya maandiko yaliyofafanua miundo na uandishi wa gazetini kupitia wanazuoni wa Tanzania.

Mwansoko (1991) alichanganua miundo mbalimbali inayotumika katika gazeteti ya Tanzania. Iligundulika kuwa katika gazeteti hujitokeza miundo ya kiisimu pamoja na kisarufi. Pia, amesisitiza kuwa baadhi ya maandishi ya gazetini waandishi hawatumii viakati vingi katika gazeteti yao. Pia, Mwansoko (keshatajwa) anasema viakati ni vijisehemu vidogo vidogo vya neno vinavyoonyesha wakati katika tendo. Anaendelea kusisitiza kuwa waandishi kutengeneza vichwa vya habari kwa kutumia vitenzi vinavyodondosha viambishi vya wakati.

Dzahene-Quarshie (2013) alichunguza lugha katika matangazo ya gazeteti ya Kiswahili nchini Tanzania. Katika utafiti wake alifafanua kwamba uteuzi wa lugha katika matangazo ya gazetini umekuwa unawavutia sio tu wanaisimu lakini pia wataalamu katika uuzaji wa gazeteti na mawasiliano. Hii ni kwa sababu uteuzi wa lugha una athari kubwa kwa matokeo ya uuzaji pamoja na kupendzesha gazeteti. Wateja wanaotuma matangazo yao gazetetini huangalia zaidi muundo na mvuto wa lugha inayotumiwa na waandishi wa gazeteti na namna gazeteti hilo linavyopata wateja.

Dzahene-Quarshie (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa magazeti ambayo lugha yake kuu ni Kiswahili matangazo yao huwa lugha ya Kiswahili na wakati mwingine kuchanganya lugha kwa kuandika Kiswahili na Kiingereza. Hii inatokana na aina ya mtangazaji na aina ya tangazo husika. Katika utafiti huu jambo hili ni muhimu kwani limeweza kutusaidia kugundua kuwa aina ya watu na mada husababisha kuwepo kwa muundo mahususi wa lugha jambo ambalo linatoa mwanga wa kuona miundo mbalimbali ya lugha inayoweza kubainika katika magazeti mbalimbali, kwa kutegemeana na uhusiano kati ya chaguo la lugha, aina ya matangazo na hadhira inayolengwa.

Utafiti wa Maina (Ht) aliyetafiti miundo ya uandishi katika magazeti ya Tanzania na kung'amua kuwa kila kampuni ya uchapishaji wa magazeti au vitabu nchini Tanzania huwa na muundo wa kuandika au kutangaza habari ambapo ni tofauti na vyombo vyingine katika matumizi ya lugha. Jambo hilo limemsukuma mtafiti kuchunguza unominishaji na utenzishaji wa maneno una tumika katika gazeti ya *Zanzibar Leo* kama kiashiria cha muundo wa uandishi kwani kategoria mbili hizi bado hazijashughulikiwa kwa mapana yake kama ilivyo.

Lusekelo (2010) alichunguza mwingiliano wa Mofolojia na pragmatiki katika magazeti ya biashara yanayochapishwa nchini Tanzania. Katika kazi hiyo anaelezea uhusiano kati ya uchaguzi wa msamiati, maumbo ya msamiati na maana zilizotarajiwa katika lugha ya matangazo ya kibiashara kwenye magazeti ya Kiswahili. Katika makala yake, amechambua kwa kiasi gani vigezo vya Mofolojia vinavyoathiriwa na pragmantiki. Matokeo ya utafiti huu yamebaini ukiukwaji mkubwa wa kanuni za ki Mofolojia na kisintaksia na badala yake kanuni za

kipragmatiki ndio huchukua nafasi. Aidha, anasisitiza kuwa maana zinazozingatia muktadha ndio hutawala uandishi huo. Anasisitiza kuwa wakati mwingine mwandishi wa gazeti hushawishiwa kutumia lugha ya Kiingereza (kuchanganya msimbo) ili kuwavuta wasomaji. Jambo hilo linatoa ithibati ya kuwa maandishi ya magazetini hutegemea kuwepo kwa miundo tofauti kutokana na jamvi/ kurasa za gazeti husika ikiwa jamvi hilo ni la michezo lugha itakayotamalaki inakuwa ni ya michezo na ikiwa ni la kitaaluma maandishi hayo yatatamalaki katika taaluma.

Pia, Lusekelo (2010) anafafanua uhusiano kati ya uchaguzi wa msamiati na ujumbe unaodhamiriwa kuifikia jamii. Katika makala yake anasema matangazo yamefikia kiwango kipyaa katika kuingiza na kutumia mifumo ya upelekaji wa ujumbe kwenye bidhaa na huduma zinazotolewa kwenye soko hivyo ni lazima matangazo yake yawe namuundo wa aina yake kwa lengo la kuivutia hadhira. Utafiti wake ni muhimu sana kwa vile unaonesha namna maandishi ya magazeti yanavyotofautiana katika nyanja tofauti kama vile biashara, michezo, na mengineyo.

Kombo (2006) alichunguza tamathali za semi katika mashairi ya magazetini nchini Tanzania. Katika uchunguzi wake alijikita katika uchunguzi wa kifani katika mashairi ya UKIMWI. Alibainisha tamathali za semi kadha zinaotumiwa na mwandishi wa mashairi katika gazeti la *Taifa Leo*. Katika utafiti huo, mwandishi aligusia miundo ya uandishi wa magazetini ambapo tunaweza kuainisha kama nimuundo au sajili ya lugha zinazoweza kujitokeza katika magazeti. Utafiti umeonesha kwamba rejista za magazetini ni miongoni mwa vipengele muhimu vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu. Katika utafiti wake alibaini kuwa kanuni za

uandishi wa mashairi zinaruhusu udondoshaji wa maneno au uchopekaji wa kiambishi ili kupata neno jipya.

2.6 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni nyenzo muhimu sana katika utafiti, uchambuzi na uhakiki wa kazi mbalimbali za kitafiti. Matumizi ya nadharia ni ya lazima katika uchambuzi wa data za utafiti. Katika utafiti huu nadharia ya Mofolojia Leksika na uamilifu zimetumika katika kukusanya na kuchambua data.

2.6.1 Nadharia ya Mofolojia Leksika

Mofolojia Leksika ni nadharia zalishi na nyambulishi inayotambua kiwango cha Mofolojia kama kiwango mahsusi cha lugha. Nadharia hii imejengwa katika misingi ya mkabala inayoitambua mofimu kama kipashio cha msingi cha kiuchanganuzi (Lieber, 1990, 1992). Nadharia ya Mofolojia Leksika inaeleza kwamba Mofolojia kama sehemu ya lugha imepangwa katika mfuatano wa ngazi kimsonge (Kiparsky, 1982; Katamba, 1993; Macmahon, 2000; Katamba na Stonham, 2006). Hii ina maana kwamba viambishi (mofimu) vinavyopachikwa katika mizizi ili kuunda neno hupangwa kidarajia. Kimsingi, nadharia hii inaonesha uhusiano wa maumbo ya maneno na sheria zinazodhibiti maumbo hayo.

Nadharia ya Mofolojia Leksika hutambua viwango viwili vya kanuni ambavyo ni kanuni Leksika ambazo huhusika katika kuunda neno kubalifu kileksika na kanuni kirai ambazo hutenda kazi baada ya neno kuundwa. Nadharia ya Mofolojia Leksika imejengwa katika mihimili mbalimbali kama vile kanuni ya ngazi leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano, kanuni ya ufinyu wa sifa na kanuni ya kuhifadhi muundo.

Msingi wa kuteuliwa kwa nadharia hii ni madai ya mhimili wa kanuni ya ngazi Leksika kwamba maneno huundwa na vipashio mbalimbali na vipashio hivyo vimepangwa katika ngazi kimsonge. Vipashio hivyo huunganishwa hatua kwa hatua na kujenga vipashio vikubwa zaidi. Hivyo basi, nadharia hii ya Mofolojia Leksika imetumika katika kubainisha na kufafanua ruwaza za ki Mofolojia katika miundo mbalimbali ya unominishaji na utenzishaji kwenye uandishi wa magazetini.

2.6.2 Mapungufu ya Nadharia ya Mofolojia Leksika

Kwa vile nadharia ya Mofolojia Leksika hutambua viwango viwili vya kanuni ambavyo ni kanuni Leksika inayohusika katika kuunda neno kubalifu kileksika na kanuni kirai ambazo hutenda kazi baada ya neno kuundwa. Kanuni hii inaonesha mchakato wa utokeaji kwake wa neno kuwa ni mchakato nasibu jambo ambalo sio sawa. Hivyo, utafiti hauwezi kujikamilisha katika kuchunguza mabadiliko ya maneno bila kutambua kanuni na sheria maalum za lugha katika mabadiliko ya maneno hayo. Hivyo, uchunguzi na uchambuzi wa data hauwezi kukamilika bila kutumia nadharia inayofafanua kanuni na kukwepa unasibu wa maneno.

Kwa hivyo, utafiti huu ulitumia nadharia ya usarufishaji ili kuweza kubaini kanuni maalumu zitumikazo katika kubadilisha kategoria za maneno.

2.5.3 Nadharia ya Usarufishaji

Wazo kuhusu usarufishaji lilionekana kwa mara ya kwanza katika kitabu cha August W. Schlegel cha mwaka 1818. Vilevile, dhana ya usarufishaji iliunganishwa katika Nadharia ya Mabadiliko ya Kisarufi na Antoine Meillet (1912) na (Lehman, 2002). Kwa mujibu wa Hickey (2010), nadharia ya usarufishaji imepata msukumo kutokana

na machapisho ya Traugott & Heine (2001) na Hopper & Traugott (2003). Nadharia ya Usarufishaji ni nadharia inayohusika na asili na mabadiliko ya maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali (Heine & Kuteva, 2005). Lengo la msingi la nadharia ya usarufishaji ni kufafanua namna maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali yanavyojitokeza na kubadilika kwa kipindi fulani pamoja na kueleza kwanini yameundwa kwa namna yalivyo (Heine na Kuteva) (keshatajwa). Misingi mikuu ya nadharia ya usarufishaji hujikita katika kutazama uelewaji wa lugha katika ujumla wake, huku ikiacha wazo la kuwa lazima lugha iwe na mipaka fulani na inahusisha vipengele vya kimuundo vya kifonolojia, kimofolojia, sintaksia na maana zake (Hansen & Drobnjakovic, 2010). Wazo la msingi katika nadharia hii ni kwamba, mchakato wa usarufishaji huchukua muda mrefu kukamilika kwa sababu mchakato huo hufanyika taratibu sana, lakini; hatimaye, mchakato huo huweza kukamilika au kutokamilika (Schiffman, 2010). Kukamilika au kutokamilika kwa usarufishaji kunatokana na sababu kwamba mchakato wa usarufishaji ni wa taratibu na una mwelekeo wa kuanzia chini kwenda juu. Mwelekeo huo hufahamika kama usarufishaji wa kidarajia (Schiffman, 2010; Lamiroy & De Mulder (2011). Hii ina maana kwamba, baadhi ya vipengele vya usarufishaji huvitangulia vingine na vingine huchelewa kufanyika. Hivyo, kutokana na kufanyika taratibu kwa mchakato wa usarufishaji, baadhi ya michakato katika lugha inaweza kuwa haijakamilika lakini ukweli ukawa michakato hiyo imechelewa kufanyika.

Kwa hiyo, kwa kuwa usarufishaji hufanyika taratibu kwa karne kadhaa lakini hatimaye hukamilika (Schiffman, 2010), tunakubaliana na kinachoelezwa na Hopper & Traugott (1993:6) wakinukuliwa na Mberi (2002) kwamba usarufishaji wa

kidarajia unaweza kuchukuliwa kuwa ni wenye kuendelea. Katika muktadha wa utafiti huu, utenzishaji na unominishaji ni mchakato wa kubainisha viambishi ambavyo vinatumika katika baadhi ya miktadha na mingine havitumiki. Kwa hali hiyo, nadharia hii ilisaidia kuainisha viambishi vya unominishaji na utenzishaji ambayo ni michakato inayoweza kufanyika kikamilifu katika mkondo wa usarufi na si vinginevyo.

2.7 Kazi Tangulizi zilizotumia Nadharia ya Mofolojia leksika na Usarufishaji

Mofolojia Leksika ni nadharia zalishi na nyambulishi inayotambua kiwango cha Mofolojia kama kiwango mahususi cha lugha. Nadharia hii imejengwa katika misingi ya mkabala inayoitambua mofimu kama kipashio cha msingi cha kiuchanganuzi. Nadharia ya usarufishaji hutumika kuangalia viwango vya kikanuni katika maneno. Watafiti kadhaa wametumia nadharia hizi katika uchambuzi wa tafiti zao.

Buberwa (2017) alitafiti Ruwaza za Ki Mofolojia za majina ya mahali ya Kihaya akiongozwa na mtazamo wa Mofolojia Leksika kwa kuchanganua vijenzi mbalimbali vinavyotumika kujenga majina ya Wahaya. Hivyo, utafiti huu umetusaidia kwa kuonena namna mofolojia inavyoweza kubadili neno kwenda katika katagoria nyingine jambo ambalo linafanana mno na miundo ya utenzishaji na unominishaji wa maneno. Pia, Shampunga (2019) alichunguza ruwaza ya kitenzi cha Kiswahili kwa mtazamo wa Mofolojia leksika. Nadharia ya Mofolojia Leksika ilitumika kufafanua miundo mbalimbali ya vitenzi vya Kiswahili, kazi hii imejadili ruwaza za ki

Mofolojia za kitenzi cha Kiswahili na kuongeza maneno kutoka katagoria moja kwenda nyingine.

Pia, Hakimu (2020) alitazama ubantuishaji wa ki Mofolojia katika vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu akiongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya usarufishaji na nadharia ya Mofolojia leksika. Nadharia ya usarufishaji ilitumika kuonesha mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza katika lugha na athari za kisarufi zinazotokana na kuingiliana kwa lugha mbili au zaidi. Nadharia ya usarufishaji ilitumika katika kuchanganua viambishi vya vitenzi hivyo.

Gromova (2020) ameandika Makala inayosomeka “mara tena juu ya suala la usarufishaji (mwana). Katika makala hii mwandishi ameitumia nadharia ya usarufishaji kwa kuonesha neno mwana linavyoweza kuambatanishwa na maneno mengine ili kutoa maana maalumu ya kikazi. Nadharia ya usarufishaji ilitumika katika msingi wa muachano wa maana ya msingi kwenda katika maana lengwa. Mtafiti amebaini kuwa neno mwana kama kijenzi ya msingi hutumiwa kuongeza neno msingi ili kubadili neno moja na jingine ingawa neno hilo linaweza kutumiwa katika maneno mbalimbali. Kimsingi utafiti huu umetusaidia kubaini namna usarufishaji unavyoweza kutoa neno moja kwenye katagoria moja kwenda nyingine.

Kwa ujumla kazi tangulizi zilizotumia nadharia za usarufishaji zinatofautiana mno na utafiti huu. Kwa sababu kazi tangulizi zilijigawa katika makundi matatu. Mosi, zilitazama ubantushaji wa vitenzi vya Kiswahili, kwa kuchunguza sifa za vitenzi vya Kiswahili na vitenzi vya kibantu katika kufanana kwake. Utafiti wetu haukuchunguza kabisa kufanana kwa vitenzi vya Kiswahili na lugha au lahaja

nyingine. Pili, tafiti tangulizi zilitazama neno msingi linavyobadilisha katagoria ya neno, utafiti huo nao unajitofautisha kabisa kwa sababu utafiti huu uliangalia kiwango cha kiambishi kinavyobadilisha katagoria ya neno na sio neno linalopachikwa kwenye neno jingine. Tatu, watafiti tangulizi walichunguza majina ya kabila ya kihaya yanavyosarufishwa ilhali utafiti huu uliaangalia mchakato wa katagoria zote unavyobadili neno kuwa nomino au kuwa kitenzi.

2.8 Pengo la utafiti

Kazi tangulizi zilitafiti miundo ya ushairi wa magazetini (Kombo, 2014; Kezilahabi, 1983), miundo ya vichwa vya habari katika magazeti (Mwansoko, 1991), uteuzi wa maneno katika uandishi magazetini (Amadi,2010), mwingiliano wa Mofolojia na pragmatiki katika magazeti ya biashara(Lusekelo,2010). Hata hivyo,eneo la unominishaji na utenzishaji wa maneno katika magazeti halijashughulikiwa. Jambo hilo lilitoa mwanya kwa utafiti huu kwa kuaangalia miundo inayotumika katika unominishaji na utenzishaji wa maneno katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

2.9 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii, mtafiti ameeleza kwa upana dhana ya rejista, maandiko kuhusu uandishi wa magazetini duniani, maandiko kuhusu uandishi wa magazetini barani Afrika pamoja na miundo ya uandishi wa magazetini nchini Tanzania. Aidha sura hii, ilijadili kwa kina mkabala wa kinadharia ambapo ulihusisha nadharia ya Mofolojia Leksika mapungufu wa nadharia ya Mofolojia leksika, nadharia ya usarufishaji, kazi tangulizi zilizotumia nadharia ya mofolojia leksika na usarufishaji sambamba na pengo la utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sehemu hii vipengele mbalimbali vikiwemo eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchanganuzi na uchambuzi wa data pamoja na uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti vimeangaziwa.

3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika Kisiwa cha Zanzibar ambapo gazeti la *Zanzibar Leo* linachapishwa na kusomwa na wananchi wake. Utafiti ulijikita katika nyanja ya isimu hasa mofolojia. Utafiti uliangazia eneo la utenzishaji na unominishaji wa maneno ya Kiswahili yanavyotumiwa na waandishi wa magazeti na hususan gazeti la *Zanzibar Leo* linalochapishwa Unguja- Zanzibar. Pili, kuwepo kwa pengo la kitaaluma kwa sababu gazeti la *Zanzibar leo* halijachunguzwa katika uga wowote wa kitaaluma. Ushahidi wa kutochunguzwa unatokana na kukosekana kwa andiko lolote linalofafanua au kuhusiana na uandishi wa gazeti la *Zanzibar leo*.

3.2 Usampulishaji wa Watafitiwa

Sampuli ni sehemu ndogo ya jamii ya watafitiwa. Hii ni sehemu ambayo mtafiti huiteuwa kwa lengo la kukusanya data. Ponera (2010) anaelezea kuwa mtafiti ndiye huamua kiwango cha ukubwa wa sampuli. Ameorodhesha baadhi ya vitu ambavyo humsababisha mtafiti kuamua ukubwa wa sampuli yake ikiwemo, aina ya utafiti, asili ya mada ya utafiti na rasilimali aliyonayo mtafiti.

Uteuzi wa sampuli ya utafiti huu umefanyika kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa Sampuli lengwa ilitumika katika uteuzi wa gazeti la *Zanzibar Leo*. Uteuzi wa Makala

ya kuchunguza katika gazeti hili zilichaguliwa kupitia sampuli nasibu, mtafiti alikata vipande vya karatasi kwa kuviweka nambari kulingana na magazeti hayo, kisha kuchaguliwa kwa mujibu wa bahati iliyoangukia ya kiuteuzi. Jumla ya magazeti kumi ya mwaka 2021 ndiyo yaliyochaguliwa katika sampuli ya utafiti huu.

3.3 Mbinu za Kukusanyia Data

Mbinu pekee iliyotumika katika utafiti huu ni mbinu ya upitiaji wa nyaraka ambazo katika muktadha huu gazeti la *Zanzibar leo* ilikuwa ni nyaraka pekee katika ukusanyaji wa data. Mtafiti alizikusanya data zote zilizopatikana katika gazeti la *Zanzibar Leo* na baadaye kuzipembua kwa mujibu wa malengo. Aidha, mtafiti alichunguza miundo iliyotumika katika utenzishaji na unominishaji maneno kwa kusoma na kuibua vitenzi na nomino zote zilizotumika kwenye habari za kisiasa na zile za michezo kisha kuchunguza miundo inayotumika katika utenzishaji na unominishaji katika magazeti kumi(10) ya mwaka 2021.

3.4 Mbinu za Uchanganuzi na Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data hauna budi uendane na malengo ya utafiti husika. Kwa hivyo, uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kulingana na malengo ya utafiti wenyewe. Data ziliwekwa katika makundi kulingana na aina ya miundo ya unominishaji na ile ya utenzishaji na kisha kutathminimuundo uliotamalaki zaidi ya mingine kati ya ile iliyoibuliwa.

3.4.1 Uchanganuzi wa Data

Data zilizokusanywa katika utafiti huu zilichanganuliwa kwa njia changamani, yaani njia ya kitaamuli na ile ya kitakwimu. Njia ya msingi iliyotumika ni ile ya kitaamuli

ambayo iliongezewa takwimu baada ya kugundua kuwa maelezo pekee yasingetosheleza kutoa taarifa. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa wakati tofauti baina ya taamuli na kuja kufuatiwa na takwimu. Mtafiti alichunguza vitenzi na nomino kadhaa vinavyotumiwa katika gazeti la *Zanzibar leo* kwa kutenzishwa au kunominishwa kwa kutumia njia za kiidadi na frikwensi na asilimia za utokeaji na baadaye kuyatolea ufafanuzi wa kimaelezo baadhi ya maneno yalichanganuliwa kitakwimu katika mijengeko yake na namna inavyobadilika katika kategoria moja kwenda nyingine.

3.5 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa matokeo ya utafiti maana yake ni hali ya matokeo ya utafiti kuwa na maelezo yenye vigezo vya kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa katika kutafitiwa huko. Kuhusu uthabiti wa utafiti ni hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayolingana na tafiti nyingine zinazolingana nazo katika siku za mbele. Vipengele hivi viwili vinabebana na kutoshelezana. Hii ikiwa na maana kuwa, ni vigumu kuwa na utafiti wenye matokeo thabiti lakini hakuna uhalali wa matokeo hayo (Kothari, 2004). Uhalali wa matokeo ya utafiti huu umethibitishwa kwa mambo yafuatayo:

Mosi, mtafiti alipata ithibati katika mamlaka ya serikali inayohusika na utafiti. Pili malengo ya utafiti yaliwekwa wazi ili kuondoa hofu wakati wa utafiti. Tatu, data za utafiti zilizokusanywa zilitumika kwa malengo ya utafiti huu, ziliepuka ubinafsi na upendeleo.

3.6 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii, tumeangalia eneo la utafiti, usampulishaji, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchanganuzi wa data, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inajihusisha na uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Sura hii itaanza na kubaini maneno yaliyonominishwa au kutenzishwa katika gazeti la *Zanzibar Leo*. kisha itawasilisha miundo mbalimbali iliyotumika katika kutenzisha na kunominisha katika gazeti hilo.

4.2 Maneno Yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa Katika Lugha ya Kiswahili

Katika uchambuzi wa matokeo ya utafiti huu, sehemu hii ilichunguza lengo la kwanza la utafiti lililohusu uainishaji wa maneno yaliyonominishwa au yaliyotenzishwa katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Utafiti huu umebaini kuwa waandishi wa gazeti la *Zanzibar Leo* hutumia maneno yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa.

Kwa ujumla maneno yaliyokusanywa yamepangwa katika makundi matatu; mosi, kundi la maneno ya asili, pili, kundi la maneno yaliyonominishwa na tatu kundi la maneno yaliyotenzishwa. Kama tulivyokwishadokeza, katika Kiswahili kuna vitenzi ambavyo vimeundwa kutokana na kategoria nyingine za maneno kwa njia ya unyambulishaji au uambishaji, mchakato ambao hujulikana kwa jina la ‘utenzishaji ama unominishaji’. Mchakato huo unaainishwa kama unavyoonekana katika Jedwali Na.4.1.

Jedwali Na. 1: Maneno yaliyonominishwa

s/n	NENO ASILI (maneno yaliyoteuliwa)	Unominishaji
1.	Andika	Andiko
2.	Baka	Mbakaji
3.	Chachu	Uchachu
4.	Chekecha	chekecheo
5.	Cheza	Mchezaji
6.	Chochea	Uchochezi
7.	Chuja	Chujio
8.	Fyeka	Fyekeo
9.	Imba	Mwimbaji
10.	Kaa	Kalio
11.	Kaanga	Kaangio
12.	Komboa	Ukombozi
13.	Legea	Ulegevu
14.	Mbaya	Mu- baya
15.	Omba	Mwombaji
16.	Pamba	Pambo
17.	Pekua	Upekuzi
18.	Pembua	Upembuzi
19.	Piga	Pigo
20.	Tamka	Tamko
21.	Tulia	Mtuliaji
22.	Ubepari	Bepari
23.	Ujinga	Mjinga
24.	Umba	Umbo
25.	Vumilia	Uvumilivu

Jedwali na 2: maneno yaliyotenzishwa

	Neno asili (maneno yaliyoteuliwa)	Utenzishaji
1.	Zawadi	Zawadia
2.	Zee	Zeesha
3.	Zembe	Zembe
4.	Zuzu	Zuzua
5.	Uma	Umiza
6.	Tobo	Toboa
7.	Tendo	Tenda
8.	Lia	Liza
9.	Pumuzi	Pumua
10.	Rasmi	Rasmisha
11.	Safi	Safisha
12.	Taifa	Taifisha
13.	Laini	Lainisha
14.	Jengo	Jenga
15.	Jumla	Jumlisha
16.	Hima	Himiza
17.	Habari	Habarisha
18.	Choko	Chokoa
19.	Duni	Dunisha
20.	Elimu	Elimisha
21.	Fupi	Fupisha
22.	Aibu	Aibisha
23.	Bora	Boresha
24.	Chafu	Chafua
25.	Uchaguzi	Chagua
26.	Choko	Chokoa

Maneno yaliyopo katika jedwali Na. 1 na 2 yalitoka katika lugha ya Kiswahili kwenye matumizi ya kawaida na kunominishwa au kutenzishwa na waandishi mbalimbali katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Yamkini, muundo ambao umeweza kubainika ni ile ya kuongeza viambishi, kunyambua au kuambisha.

Masamba na wenzake (2003) wanasema kuwa viambishi nyambuaji au ambatanishi vinaweza kutumika kama msingi wa kubadili kategoria ya neno. Jumla ya maneno 25 yamenominishwa sawa na asilimia 47 ya jumla ya maneno yote. Pia, maneno 26 yametenzishwa sawa na asilimia 53 ya jumla ya maneno yote.

4.3 Miundo Iliyotumika katika Unominishaji wa Maneno

Katika sehemu hii mtafiti anachambua lengo la pili la utafiti wake ambalo ni kuchambua miundo ya utenzishaji na unominishaji iliyojitokea katika gazeti la Zanzibar leo. Aidha, Sehemu hii itanza kufafanua kwa ufupi miundo iliyojitokeza katika unominishaji wa maneno. Aidha, uchambuzi wa kila muundo utaonekana kwenye jadwali la muundo husika.

Jedwali Na. 3: Orodha ya Miundo Iliyominishwa

	Kategoria Za Maneno	Miundo Wa Unominishaji	Idadi Ya Maneno	Asilimia
4.2.1.1	Vitenzi vyenye kutoa amri	{MU, M} + SHINA- KT+ {JI}	06	24.5
4.2.1.2	Vitenzi vya kibantu vyenye kuishia irabu {a}	MZ+KTM{O}	07	29.5
4.2.1.3	Vitenzi vyenye kuanza na konsonenti	U+SN+ KTMKNz	06	24.52
4.2.1.4	Sifa/vivumishi	Mu+SN U+SN Q+SN M+SN	05	20
4.2.1.5	Vitenzi amri	{KU}+SH		

Utafiti huu umebaini miundo iliyotumika kunominisha maneno katika gazeti la *Zanzibar Leo*. jedwali Na: 4.2 linaonesha miundo hiyo, ambayo ilifafanuliwa kwa uwazi katika maelezo yanayofuatia hapo chini. Aidha katika miundo ya unominishaji kwenye gazeti hili kategoria za vitenzi ndizo zilizonominishwa kwa asilimia 80 na asilimia 20 yalitoka kwenye kategoria ya sifa yaani kivumishi na kiwakilishi. Kujitokeza kwa kategoria moja kwa wingi ni miongoni mwa kanuni inayokubaliwa na wananadharia ya usarufishaji kama waliyosema Schiffman (2010 na Lamiroy & De Mulder (2011). Baadhi ya vipengele vya usarufishaji huvitangulia vingine na vingine huchelewa kufanyika. Hivyo, kutokana na kufanyika taratibu kwa mchakato wa usarufishaji, baadhi ya michakato katika lugha inaweza kudhaniwa haijakamilika lakini ukweli ukawa michakato hiyo imechelewa kufanyika. Katika utafiti huu imebainika kuwa yapo maneno kadhaa yanayoweza kunominishwa kutoka katika kategoria mbalimbali za maneno. Miongoni mwa miundo iliyotumika kunominisha na kama ilivyoainishwa hapa chini.

4.3.1 Muundo wa Kiambishi awali {mu, m} + shina- KT+ kiambishi tamati {ji}

Utafiti umebaini kuwa nomino hizi zimetumika katika gazeti la *Zanzibar Leo* kwa kutumia muundo au fomula maalumu ambayo ni *Kiambishi awali cha nomino {mu, m} + shina- KT+ kiambishi tamati {ji}* chenye sura ya unominishi. Kwa kuongezeka kiambishi tamati {J} ndio hufanya msisitizo wa unominishaji. ⁵.muundo huu umejidihirisha kwa asilimia 24.5 ya jumla ya maneno yote yaliyonominishwa. Nomino hizi zimeingia katika kundi la kitenzi na kuipeleka kwenye nomino kwa kuainisha kazi wazifanyazo watu wenye tendo hilo. Katika habari za michezo neno

⁵ *Zanzibar Leo* 07/02/2021

mchezaji lilitawala sana. Neno ‘imba’ lilinominishwa kwa kutumia hali/mitindo miwili.

Mosi, kanuni ya uimarikaji wa fonimu hutokea kwani umbo la ndani la kitenzi ‘imba’ wakati likinominishwa kuwa mwimbaji ni *mu+i+mba+ji*. Hapa fonimu u+i zimeimarika na kuifanya nusu irabu /w/ na kuwa irabu nzito.

Pili, neno hili hujitokeza kwa muundo wa kishazi nomino, kwa mfano ‘uimbaji; yaani *u+i+mba+ji* hapa inaoneka {u} pamoja na kiambishi tamati {ji} kufanya kazi ya kunominisha. Kwa mfano, *kamati ya utendaji TUSA kukutana Februari*. Mfano ufuatao unadhihirisha ufafanuzi huo.



Kielelezo Na.1: Mfano wa Unominishaji

Katika mfano huo kwenye kichwa cha habari, neno “kua” limepachika {u} kikiwa ni kiambishi awali na {ji} ya kiambishi tamati kinominishi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mofolojia leksika, kuna viwango viwili vya kanuni ambavyo ni kanuni Leksika ambazo huhusika katika kuunda neno kubalifu kileksika na kanuni kirai ambazo hutenda kazi baada ya neno kuundwa, maneno hayo yote yamefuata misingi madhubuti ya nadharia ya Mofolojia leksika. Mifano inaonekana katika jedwali Na.3 inabainisha miundo ya unominishaji inayotumika katika gazeti la *Zanzibar Leo*

Jedwali Na. 4: Miundo ya unominishaji m/mu+sh+ji

s/n	Kategoria asili	Mtindo uliotumika kunominisha{mu, m} + shina- KT+ kaiambishi tamati {ji}
1	Cheza	M+chez+a+ji
2	Chora	M+chor+a+ji
3	Tangaza	M+tangaza+ji
4	Imba	Mwimbaji au uimbaji
5	Winda	Mwindaji
6	Ua	Mu+ua+ji

Katika jedwali namba 3. jumla ya maneno 06 yalibainika kutumiamuundo wa {mu, m} + shina- KT+ {ji} kaiambishi tamati} ambapo ni sawa na asilimia 24.4 ya maneno yaliyoteuliwa kuchunguzwa kupitia miundo ya unominishaji iliyotumika katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Ingawa katika neno “ imba” na kuwa “mwimbaji” lilipaswa liwe ‘muimbaji’ lakini mara nyingi masharti zuizi ya lugha yanaweza kujitokeza katika kudhoofisha na kunyenyusha irabu mbili na kufanya konsonanti moja. Hii inatokana na kanuni za kimatumizi katika jamii na ndio maana baadhi ya muda katika kanuni za kisarufi zimeachwa. Kwa mfano, Mgullu (2012) anasema irabu /u/ inaweza kubadilika na kuwa nusu irabu /w/ kama neno ‘mueusi= mweusi’.

Kwa ujumla waandshi na wahariri wa gazeti la *Zanziba Leo* wanaonesha kutumia kanuni za uundaji wa maneno bila kujua kama wanafuata kanuni hizo. Wahariri watano waliododoswa walisema hawajui kwanini maneno yanabadilika katika kategoria za maneno kwa miundo hiyo.

Masamba na wezake (wameshatajwa) nomino zilizoingizwa kiambishi {ji} ni nomino zilizonyambuliwa kutoka katika vitenzi na kuonesha hali ya urudiaji wa tendo. Na pia, vinabeba sifa ya unyambuaji wa neno. Nomino zinazoundwa na kiambishi awali cha unominishi cha {m} au {mu} pamoja na kiambishi tamati {ji} vinaweza kuwa nomino zinazoonisha kazi aifanyayo mtu (Mgulu: 2012.)

4.3.2 Muundo wa Unominishaji unaotokea kwa vijenzi vya Mz+o (kt)

Utafiti umebaini kuwa unominishaji unaweza kujitokeza iwapo vitenzi vyenye asili ya kibantu ambayo vinaishia na irabu {a} vinaweza kubadilika katika kategoria hiyo na kuwa nomino pale zinapopachikwa irabu {o}. Muundo huu umeweza kujitokeza katika maneno 07 kati ya maneno 27 yaliyonominishwa ambayo imechukua jumla ya asilimia 25 ya maneno yote yaliyonominishwa. Mifano mbalimbali iliyogunduliwa katika gazeti hili inaonekana katika jedwali 4. Kwa mujibu wa nadharia ya mofojojia Leksika inafafanua kuwa viambishi (mofimu) vinavyopachikwa katika mizizi huunda neno na kupangwa kidarajia. Kimsingi, nadharia hii ilionesha uhusiano wa maumbo ya maneno na sheria zinazodhibiti maumbo hayo. Kama inavyoonekana katika maandishi ya gazeti la *Zanzibar Leo*.

Jadwali Na. 5: unominishaji wa Kutumiamuundo wa Mz+ktz+o

s/n	Kitenzi cha Asili	Mtindo wa unominishaji
1	Pamba	MZ+KTM{O} = Pambo
2	Piga	MZ+KTM{O}=Pigo
3	Pinda	MZ+KTM{O}=Pindo
4	Soma	MZ+KTM{O}=Somo
5	Tangaza	MZ+KTM{O}= tangazo
6	Umba	MZ+KTM{O}=Umbo
7	Tamka	MZ+KTM{O}= Tamko

Utafiti ulibaini kuwa katika kategoria ya unominishaji kama ilivyoanishwa katika jedwali na 4, jumla ya asilimia 29.5 ya maneno yaliyokusanywa yalitumiamuundo huu. Kwa ujumla kategoria hii imebaini kuwa ina sifa ya umoja wa kidhahania $\{Q+Mz+o\}$ na wingi wake hutumia kiambishi $\{ma\}$. Kwa kawaida vitenzi vingi vinavyoishia na irabu $\{a\}$ vinaweza kuingizwa irabu $\{o\}$ na kubadilika kategoria ya kitenzi kwenda nomino. Kwa mfano, neno $Pamb+a$ linaweza kuwa $Pamb+o$. Katika gazeti la *Zanzibar Leo* limetumika neno *tamko*⁶ kwa kusema *ZFF yatoa tamko kuhusu udhamini wa pombe ligi ya Zanzibar*. Hapa neno tamko limenominishwa kwa kutumiamuundo wa upachikaji $Mz+ktm\{o\}$ na kupata kategoria ya nomino. Kwani neno hilo linaweza kutolewa katika kategoria ya kitenzi “tamka”. Waihiga (2011) anasema kwamba kiambishi $\{o\}$ hutumika kwa wingi. Pia Habwe na Karanja (2004) wanasema katika kuunda nomino kutoka katika vitenzi. Nomino hizo huleta dhana ya kitu au kifaa kinachotumika. Pia, nadharia ya Mofolojia Leksika hutambua viwango hivyo vya kikanuni na ilibainisha viwango viwili vya kanuni ambavyo ni

⁶Gazeti la Zanzibar leo la tarehe 9/7/2021

kanuni leksika na kirai ambazo hutenda kazi baada ya neno kuundwa na huhusika katika kuunda neno kubadilika kileksika.

4. 3.3 Muundo wa Unominishaji wa kijenzi U+Mz+ zi

Baadhi ya maneno yamebainika kunominishwa kwamuundo wa kutumia kiambishi cha unominishi {u} pamoja na mzizi wa neno ukifuatiwa na kiambisi tamati maana {z}. Nomino hizo huchukua kijenzi cha {u} na {zi} kama kijenzi cha msingi cha unominishaji. Maneno yenyemuundo wa aina hii yamechukua asilimia 24.4 ya maneno yote yaliyonominishwa. Pia, kategoria hili imeweza kutumia kiambishi Vi+shina+viambishi tamati vijenzi unominishi. Kwa mfano, *Mourinho atoa visingizio*⁷ vichapo spurs. Hapa neno visingizio limetokana na neno singizia ambalo kiasili ni kitenzi ila lilipobadilika na kufuatamuundo wa vi+mzizi+ktm+ktkn lilibadilika moja kwa moja kutoka kategoria moja kwenda nyingine. Mifano mingine iliyogundulika katika gazeti la *Zanzibar Leo* ni:-

- “*Bunge lataka ukaguzi dampo la nduba*”⁸
- “*Ghasia zazuka uchaguzi mdogo*”⁹ “*Othman: nitawatumikia wazanzibar bila ubaguzi*”. (ZL: 3 Machi, 2021.Uk.1)

Hiyo ni baadhi ya mifano iliyochambuliwa katika sentensi nzima lakini ifuatayo katika jedwali Na.6 ni mifano michache iliyochukuliwa kutoka gazeti la Zanzibar leo kama neno moja la msingi ili kuonesha miundo inayotumika katika unominishaji wake.

⁷ Gazeti la Zanziabr leo la Jumapili ya 7/02/2021

⁸ ZL: 5 MACHI 2021. UK. 16

⁹ ZL: 5MACHI2021. UK.16

Jedwali Na. 6: Maneno yaliyonominishwa kwa kutumiamuundo**U+Sn+KTMKNz**

s/n	Kitenzi Asili	Mtindo Ulionominishwa
1	Chagua	U+SN+ KTMKNz = Uchaguzi
2	Chochea	U+SN+ KTMKNz = Uchochezi
3	Pekua	U+SN+ KTMKNz = Upekuzi
4	Pembua	U+SN+ KTMKNz = Upembuzi
5	Komboza	U+SN+ KTMKNz = Ukombozi
6	Fafanua	U+SN+ KTMKNz = Ufafanuzi

Ni wazi kuwa, kiambishi “u” awali na “zi” tamati maana vimeweza kunominisha vitenzi kwa kubadilisha kategoria ya neno husika kama ilivyoonekana katika jedwali Na.5. baadhi ya wataalamu kama vile, Waihiga (2011) na Mgullu, (2012) wanashadidia muundo huu kuwa unaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha ya Kiswahili, kwa kusema iwapo mzizi wa neno unaanza kwa irabu, kiambishi {u} hutumika katika kuitambulisha nomino. Nomino nyingi za udhahania katika lugha ya Kiswahili hunominishwa kwa kutumia kiambishi awali {u} na kuishia kiambishi tamati {zi}. Maneno ya wataalamu hawa yamejidhihirisha kwenye mifano iliyopo kwenye jedwali Na. 6 hapo juu.

4.3.4 Muundo wa Unominishaji kwa maneno yanayotokana na sifa

Utafiti umebaini uwepo wa nomino zilizotokana na vivumishi vya sifa ambavyo havinamuundo mmoja wa upachikaji wa viambishi vyake katika kuiendea kategoria hiyo. Nomino hizi zimejitokeza kwa asilimia 20 kati ya maneno yote yaliyonominishwa. Hivyo ni wazi kuwa lugha inaweza kujengeka kwa masharti zuizi yaani neno moja kuwa na masharti yake na jengine kuzuiliwa kuingia katika

masharti hayo. Hivyo, kategoria ya neno inaweza kuwa moja lakini masharti ya kufikia kategoria hiyo ikawa ni tofauti. Masamba (2016) anaeleza kwamba kuwa masharti zuizi ni kigezo kinachotumika kuamulia ukubalifu wa mofimu zinazounda kundi fulani. Kwa vile utafiti umetumia nadharia ya mofimu leksika ubadilishaji wa mofimu katika kutengeneza neno katika kategoria moja hazitokuwa na tatizo lolote kwa sababu nadharia hii inakubaliana na muundo huo ikiwa utajitokeza katika neno.

Heine na Kuteva (2005) wanasema misingi mikuu ya nadharia ya usarufishaji hujikita katika kutazama uelewaji wa lugha katika ujumla wake huku ikiacha wazo la kuwa lazima lugha iwe na mipaka fulani na inahusisha vipengele vya kimuundo vya kifonolojia, kimofolojia, sintaksia na maana zake. Utafiti umebaini kuwa waandishi katika gazeti la *Zanzibar Leo* huandika maneno yenye utaratibu kama huo kama yanakavyoonekana katika jedwali Na. 6.

Jadwali Na.7 :muundo inayofuata masharti zuizi

S/n	Sifa (vivumishi)	Nomino
1	Mbaya	Mu+SN= Mu- baya
2	Chachu	U+SN= Uchachu
3	Ubepari	Q+SN= Bepari
4	Ujinga	M+SN= Mjinga

Kwa mujibu wa vikundi sifa zilizobainishwa hapo juu ni wazi kuwamuundo wa unominishaji katika vikundi sifa hivyo ilitofautiana katika upachikaji wa kiambishi awali cha unominishi. Hata hiyo katika mgao wa kategoria yamuundo huu yapo baadhi ya maneno yaliyovuka urazini wa kikanuni kama zilivyotajwa na kwa mujibu wa masharti zuizi ya neno husika maneno hayo hayakujitokeza katika fomula ya

moja kwa moja kama muundo huo ulivyoonekana katika jedwali Na.7 la hapo juu. Kwa mfano, neno sifa “dhalili” haikufuata mpango huu bali ilichukua {U} KN+mz+Ktm+KN {ji} = udhalilishaji. Kwa mfano, *watakiwa kushirikiana kukomesha udhalilishaji* (ZL3 Machi. 2021. Uk. 3). Mfano mwingine ni “udhamini” kama itakavyobainishwa na kielelezo hapa chini.



Kielelezo Na.2: Mfano wa unominishaji wa ‘Taratibu’

Kama inavyoonekana kwenye kielelezo, neno “utaratibu” katika kichwa cha habari kilichokeleza wino hapo juu ni sifa iliyopachikwa kiambishi awali {u} na kuwa nomino.

4.3.5 Upachikaji wa kiambishi {o} tamati kwenye vitenzi vinavyoishia na kiambishi {-a} tamati

Baadhi ya maneno yanayoishia kiambishi {a} huweza kubadilika kategoria ya kitenzi pindi kinapopachikwa kiambishi tamati {o}. Hata hivyo, kuna baadhi ya vitenzi vya kibantu ambavyo huishia na kiambishi tamati {-a} ambavyo vikiambikwa viambishi tamati {-o} haviwezi kubadilika na kuwa nomino. Kwa mfano, vitenzi ‘lowa’, na ‘tembea’ vinazuiliwa na kanuni ya masharti zuizi yanayoifanya lugha kuwa na ukinzani butu wa kikanuni ambapo kanuni hizo hizo kuna wakati huwa hazifanyi kazi katika kifungu cha maneno husika. Utafiti umebaini kuwa katika gazeti la *Zanzibar Leo* vipo vitenzi vinavyotumia muundo wa Mz+Sh+a na kubadilika kuwa kategoria nyingine yenye muundo wa Mz+Sh+a {o}, kama mifano hii inavyodhihirisha

Jadwali Na. 8: mifano inayonominishwa kwamuundo wa Mz+Sh+a

Mtindo wa Mz+Sh+a		Mtindo wa Mz+Sh+a
Kitenzi	Mzizi + o	Nomino
Tenda	tend + o	Tendo
Andika	andik + o	Andiko
Jenga	jeng + o	Jengo
Pamba	pamb + o	Pambo

Kitenzi kinachoundwa na mzizi wa neno ulioishia na kiambishi tamati maana {a} unaweza kubadilika kategoria kutoka kitenzi na kuwa nomino pale unapobalishwa na kiambishi tamati maana {o}. Ushahidi wa maelezo hayo unajidhihirisha katika jedwali la 7 hapo juu.

4.3.6 Maneno yaliyonominishwa kwamuundo wa m + {-i/-li-} + {-o }

Utafiti ulibaini katika gazeti la *Zanzibar Leo* kutumika baadhi ya vitenzi ambavyo kiambishi cha unyambulishi {-o} huweza kunyambulisha nomino kwa kuambatana na kinyambulishi {-i} au {-li}. Kwa mfano, mzizi wa neno hufuatiwa na kiambishi {-i/-li-} + {-o} kinyambulishi na kuibadilisha kategoria ya kitenzi na kuifanya kuwa nomino yenye kazi ya utendaji, kama mifano hii kutoka *Zanzibar Leo* inavyoonesha katika Jedwali Na. 9 hapo chini. Mchakato huo umefanyika kwa kupitia msingi mkuu wa nadharia ya usarufishaji ambao unatazama mabadiliko ya maumbo ya maneno yanayotokana na watumiaji wa lugha kutumia mabadiliko yanayowafanya waweze kufahamiana katika matumizi ya lugha yao.

Jedwali Na. 9: Maneno yaliyonominishwa kwamuundo wa m + {-i/-li-} + {-o }

Kitenzi	Mzizi	Nomino
Kaanga	kaang + i + o	Kaangio
Chuja	chuj + i + o	Chujio
Kaa	ka + li + o	Kalio

Katika mazingira mengine kiambishi kinyambulishi {o} huweza kunominisha kitenzi pale kinapoaambatana na mofimu {e} {Mzizi+} + {-e-} + {-o}. Miundo hii nayo imegunduliwa kutumika katika gazeti hili kama inavyoonekana katika jedwali namba 9 hapo chini. Hata hivyo, muundo huu haukutumika kwa maneno mengi kwani umegundulika kwa maneno mawili (02) sawa na asilimia mbili (02) katika jumla ya maneno yaliyotafitiwa. Mifano hiyo inajidhihirisha katika jedwali Na. 10 hapo chini

Jedwali Na 10 : Maneno Yaliyonominishwa Kwamuundo wa {Mzizi+}

+ {-e-} + {-o}

Kitenzi	Mzizi + viambishi vinominishi	Nomino
Fyeka	fyek + e + o	Fyekeo
Chekecha	chekech + e + o	chekecheo

Muundo huu haukujitokeza sana katika maneno mengi yanayoandikwa kwenye gazeti la *Zanzibar Leo*. Watafitiwa walipouliza sababu ya kutokuwa na maneno mengi waliashiria kuwa kanuni za maneno yenyewe katika lugha haikubali kuyageuza maneno mengi yatumikayo katika Kiswahili fasaha. Hata hivyo asilimia 02 ya maneno yote bado inatupa nafasi ya kusema kuwamuundo huu ni miongoni mwa miundo inayotumika katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

Mochiwa (2007) katika utafiti wake amekiri kuwa maneno yenye kuishia irabu ,o> au kuwa na irabu <o> fuatizi ni machache mno katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa utafiti wake anabainisha maneno mawili tu nayo ni <soga> kwa <sogoa> na bomo kuwa <bomoa>. Hata hivyo maneno hayo aliyoyatoa kama mfano hatukuyaona popote katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

4.3.7 Kupachika kiambishi {ku} ya unominishi

Baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vinaweza kupachikwa kiambishi {ku} kinominishi na kubadilika hadhi kuwa nomino. Kiambishi hiki {ku} huwekwa mbele ya shina la kitenzi. Kwa kufanya hivyo hubadili kitenzi kuwa nomino. Katika gazeti la *Zanzibar Leo* kumegunduliwamuundo huu wa unominishaji kama ulivyo katika kanuni za lugha ya Kiswahili. Kupitia nadharia ya usarufishaji inayohusika na asili na

mabadiliko ya maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali (Heine & Kuteva, 2005). Mwandishi wa *Zanzibar Leo* umefanikiwa kufuata kanuni hii. Kwa sababu lengo la msingi la nadharia hii ni kufafanua namna maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali yanavyojitokeza na kubadilika kwa kipindi fulani pamoja na kueleza kwanini yameundwa kwa namna yalivyo. Katika gazeti la *Zanzibar Leomuundo* huo umetumika mno, kwa kupachika vimbishi vinavyobadili hali kidaraja. Hata hivyo, nomino hizi bado zinabaki na umbo lake la asili la kuwa kitenzi lakini hadhi yake ya kikazi hugeuka na kuwa nomino. Kwa mfano, iliyoonekana katika gazeti hili inaoneshwa katika jedwali namba kumi hapo chini.

Jedwali Na. 11: Mifano ya unominishaji wa kiambishi “ku”

Kitenzi	“Ku” kinominishi+ shina	Nomino
Imba	ku + imba	Kuimba
Cheza	ku + cheza	Kucheza
Lia	ku + lia	Kulia
Piga	ku + piga	Kupiga

Mtindo huu umebainika kujichomoza katika gazeti la *Zanzibar Leo* kwa jumla ya maneno manne (04) kati ya maneno yote yaliyochunguzwa na kujenga asilimia saba 07 ya jumla ya maneno yote yaliyotafitiwa. Waihiga (keshatajwa) anakubaliana na kiambishi {ku} kuwa kinaweza kunominisha kwa kusema, nomino za kundi hili huundwa na vitenzi. Kiambishi {ku} hutokea mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi.

4.4 Muundo ya Utenzishaji wa Maneno Kutoka Katika Gazeti la Zanzibar Leo

Sehemu hii pia, inajibu lengo la pili la utafiti linalotaka kubaini miundo iliyotumika katika utenzishaji wa maneno katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

Utenzishaji ni mchakato wa kubadili kategoria moja ya maneno kuwa kitenzi¹⁰. miundo ya utenzishaji iliyotumika katika gazeti la *Zanzibar Leo* ni kama inavyoainishwa katika Jedwali Na.12.

Jadwali Na. 12: Orodha ya muundo Iliyotumika Kutenzisha

Namba	Aina ya kiambishi	Kanuni	Idadi ya vitenzi katika gazeti vyenye kanuni hii	Asilimia
4.2..1	-esh na ish	MZ/S+KJ+K/KS MZ/S+KJ+KK	06	15.3%
4.2.2	-ka-	MZ/S+KJ+KKS	04	10.2%
4.2.3	Isha	SH+isha	07	17.9%
4.2.4	nomino {sh+i}	sh+i}	04	10.2%
4.2.5	Vivumishi {isha}esh}	SH+ish/esha	04	10.2%
4.2.6	- izi-	KnyTz+ iz	03	7.6%
4.2.7	Nyambuo Tenzishi – a	SH+kfTsh	07	17.9%
4.2.8	Iza Ka A Ku		04	10.2%
Jumla			39	100%

4.4.1 Utenzishaji wa viambishi vya unyambuaji -esh na -ish

Utafiti umebaini kuwa viambishi nyambuaji {esh} na {ish} vinakaribiana mno katika kutenzisha maneno kwa sababu mara nyingi huwa vinatenzisha kategoria moja ya

¹⁰ Elizeus G. Katikiro (2017) Tathmini ya Mchakato wa Utenzishaji katika Kiswahili na Hadhi ya Msamiati wake Kikamusi katika jarida la mtandaoni. African Journal online.

neni na hasa huwa zinaenda moja kwa moja kwenye sifa au vivumishi vya sifa. Mtafiti amebaini kuwa waandishi wa *Zanzibar Leo* wanatumia muundo huu sana. Jumla ya maneno 07 sawa na asilimia 13 katika jumla ya maneno yaliyotafitiwa yametumia muundo huu.

Jedwali Na . 13: Muundo wa utenzishaji wa viambishi vya unyambujaji –esh-

Sifa ya Asili	Mtindo wa Utenzishaji	Kitenzi zalishi
Bora	MZ/S+KJ+K/KS	Boresha
Zee	MZ/S+KJ+K/KS	Zeesha
Duni	MZ/S+KJ+K/KS	Dunisha

Vile vile, katika kategoria hiyo hiyo na kwa msingi huo huo gazeti la *Zanzibar Leo* limetumia muundo wa unyambujaji unaobebwa na {ish}+a unachukua sura ya utenzishaji kama unavyodhihirika katika mifano kwenye Jedwali Na. 13 hapo chini.

Jedwali Na .14 : mifano ya utenzishaji kwamuundo wa – ish+a

Sifa	Mtindo wa utenzishaji	Kitenzi
Fupi	MZ/S+KJ+KK	fupisha
Safi	MZ/S+KJ+KK	safisha
Laini	MZ/S+KJ+KK	lainisha

Pia, Utafiti umebaini kuwa viambishi nyambuo tenzishi –{esh-} na {-ish-} ni vipachio vinavyoonesha utendeshi wa jambo miundo huu umechukua jumla ya 15.3% ya utenzishaji katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Kiambishi fuatishi tenzishi <a> pia hutumika kuunda vitenzi kutoka kwenye maneno ambayo kategoria si kitenzi. Irabu <a> . Mochiwa (2007) katika maneno ya Kiswahili <a> ni irabu ishilizi kitenzi katika maneno mengi yenye asili ya kibantu hivyo, kutokea kwa maneno ya kutoka

kategoria tofauti yanaweza kuwa kitenzi. Katika utafiti wake anaonesha wazi maneno yanayoweza kujibadilisha kama vile <zawadi> kuwa <zawadia>, <kombo> kuwa <komboa>

4.4.2 Utenzishaji wa kiambishi {- k- }cha k/utendeka

Utafiti umebaini kuwa katika gazeti la *Zanzibar Leo* waandishi walitumia vitenzi vilivyotenzishwa kutoka kategoria ya sifa/ kivumishi kuwa kitenzi chenye kauli ya utendeka. Vitenzi vilivyobainika ni vile vinavyopachikwa {u} kwenye mzizi kama kiambishi kinachosaidia mzizi wa neno na hapo hapo hufanya kazi ya utamati maana na kufuatiwa na kiambishi {ka} cha utendeka. Jumla ya 10.2% ya maneno yote yaliyotenzishwa yamejidhihirisha katikamuundo huu. Mifano ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Jadwali Na. 15 muundo wa utenzishaji kwa kufuata MZ/S+KJ+KKS

Sifa/ kivumishi	mchakato wa utenzishaji	kitenzi zalishi tendeka
Chafu	MZ/S+KJ+KKS	chafuka
Pevu	MZ/S+KJ+KKS	pevuka
Erevu	MZ/S+KJ+KKS	Erevuka
Refu	MZ/S+KJ+KKS	Refuka

Maneno yaliyoonekana katikamuundo huu ni maneno yenye sifa na yanayoishia irabu {u} na kuchukuamuundo wa MZ/S+KJ+KKS ambapo kiambishi “ka” kimefanya kazi ya kiambishi tamati maana utenzishaji wa hali. Kiango (2000) anasema kuna vinyambuo vya vitenzi vinavyojitokeza katika maneno yenye sifa ya kivumishi ik, ek, na k, vinyambuo hivi vinaweza kufanya vitenzi tendeshi kutoka

katika asili ya vivumishi sifa kwenye maneno kama vile < zee> kuwa <zeeka> < laini> kuwa <lainika>

4.4.3 Utenzishaji wa vipashio vya {-isha} kutoka katika nomino

Kiambishi fuatishi tenzishi -ish- kimebainika kuchopekwa mno katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Muundo huo umezitumia nomino zinazoishia na irabu. Kiambishi huchopekwa katika nomino hizo na kuibadilisha taswira ya unomino na kuifanya kuwa tenzishi kwenye nomino zinazotokana na nomino za msingi katika muundo wake. Aidha, katika mifano iliyoorodheshwa hapo chini, kiambishi tenzishi -ish- kina uwezo mkubwa wa kubadili kategoria mbalimbali za maneno kuwa kategoria ya kitenzi. Mifano inajidhihirisha katika jedwali namba 14 hapo chini.

Jedwali Na. 16; muundo wa utenzishaji kwa kufuata Mz+ish+kt

Nomino	Mtindo wa utenzishaji	Kitenzi
Taifa	Mz+ish+kt	Taifisha
Elimu	Mz+ish+kt	Elimisha
Aibu	Mz+ish+kt	Aibisha
Habari	Mz+ish+kt	Habarisha
Rasmi	Mz+ish+kt	Rasimisha
Safiri	Mz+ish+kt	Safirisha
Jumla	Mz+ish+kt	Jumlisha

Utafiti umebaini kuwa mchakato wa utenzishaji unaotokana na nomino zenye kuishia irabu ya {a, e na u} umechukua asilimia 17.9 ya maneno yote yaliyotenzishwa katika gazeti la *Zanzibar Leo*.muundo huu umejidhihirisha katika nomino tu na sio kwenye

aina nyingine za maneno. Nomino hizo zimepachikwa kiambishi tamati maana <i> na kiambishi kauli ya kutendesha <sha>

4.4.4 Muundo wa Utenzishaji unaotokana na nomino {sh+i}

Utafiti umebaini kuwa baadhi ya maneno yanayotenzishwa katika lugha ya Kiswahili ni yale yanayopachikwa irabu yenye kazi ya kiambishi tamati maana kitenzishi {i}. Maneno mengi yanayopachikwa irabu hiyo ni maneno yenye asili ya lugha ya kiarabu. Utafiti umebaini kuwa waandishi katika gazeti la *Zanzibar Leo* walichukua maneno hayo na kupachika irabu mwisho wa neno irabu ambayo hubadili taswira zima ya neno pamoja na kategoria yake. Jumla ya asilimia 10.2 ya maneno yaliyotenzishwa yaligunduliwa kuwa katika kategoria hii.

Jedwali Na.17 muundo wa utenzishaji kwa kufuata Sh+Ir

NOMINO	KITENZI Sh+Ir
Shitaka	Shitaki
Sifa	Sifu
Sitaha	Sitahi
Subira	Subiri

Kwa ujumla mizizi ya nomino hizi ni ile yenye asili lugha ya kiarabu ambayo yameletwa kwenye ubantu ambapo irabu {a} kubadilika na kuwa {i} kama kiambishi tamati maana kitenzishaji.

Mochiwa (2007) kiambishi <i> kianaweza kuwa kiambishi tamati maana na kuweza kubadili neno kuwa kitenzi, pia, kinaweza kuwa kiambishi fuatishi kinachodokeza

mofimu ya utenzishi kwa mfano, <hadithi> linaweza kuwa <hadithia> na <dhamira> kuwa < dhamiria>

4.5.5 Muundo wa utenzishaji unaotokana na Vivumishi

Mtafiti amebaini kuwa viambishi {-isha}, na {esha: vimebadili kategoria ya uvumishi na kuifanya kuwa tendo. Jumla ya asilimi 10.2 ya maneno yote yaliyotenzishwa yalibainika. Miongoni mwa maneno yaliyobaini ni:-

Jedwali Na.18: Muundo wa utenzishaji unaotokana na Vivumishi

Kivumishi	Mtindo unaofuata kanuni ya <sha, isha, na esha	Kitenzi
Refu	sha	refusha
Fupi	isha	fupisha
Bora	esha	boresha
Safi	isha	safisha

Mabadiliko ya kategoria hayakufanana kwa asilimia mia bali yalitofautiana kulingana na asili ya neno husika na ndio maana viambishi tamati maana vikiwa tofauti na viambishi tamati vikiwa vina uwiano sawa kutoka kila kategoria moja ya neno. Jambo hilo ni la kisarufi na linakubaliwa na nadharia ya usarufishaji kwenye msingi yake. Aidha, vitenzi vinaweza kuundwa kutokana na vivumishi. Katika taaluma ya isimu ya uundaji wa maneno leksimu moja inaweza kuingizwa viambishi na kupata maumbo tofauti na umbo la neno la awali (Matinde: 2012).

4.4.6 Kiambishi Nyambuo Tenzishi –a SH+kfTsh

Utafiti umebaini kuwa kiambishi fuatishi tenzishi {a} kimetumika katika gazeti la *Zanzibar Leo* katika utezishaji wa maneno. Katika mifano imebainika kuwa irabu ‘a’

ina dhima ya kutenzisha maneno msingi. irabu hii hujitokeza mwishoni mwa neno na kuwa kiambishi tamati maana. Pia irabu {a} katika vitenzi vilivyochunguzwa imebainika kujenga sifa ya utendeshi katika kitenzi cha Kiswahili. maneno yaliyotumika kwamuundo huu ni asilimia 17.9 ya idadi ya maneno yote yaliyotenzishwa na jedwali Na.16 hapo chini linaonesha mifano ya kategoria hii.

Jedwali Na. 19 : Miundo ya utenzishaji kwa kutokea kategori tofauti

Aina ya neno	Neno asili	Kitenzi unde
Nomino	Tobo	Toboa
Nomino	Zuzu	Zuzua
Kivumishi	Chafu	Chafua
Nomino	Pumu	Pumua
Kivumishi	Zembe	Zembea
Nomino	Zawadi	Zawadia
Nomino	Choko	Chokoa

Mtindo huu wa nyambulishi tenzishi unaofuata kanuni ya {-a SH+kfTsh,} umejidhihisha katika maumbo tofauti ya maneno yapo yanayomalizia {ao,{ia}, {ua} na {oa} muishio huu unaonekana ni tofauti kwa umbo lakini unafanya kazi moja, ambayo ni utenzishaji.muundo huu umefuata msingi ya nadharia ya Mofolojia Leksika ambapo mchakato wa utenzishaji umetambua kwa kupitia viwango viwili vya kanuni za uundaji wa maneno na kuyaweka katika kategoria tofauti ambayo ni kanuni ya Leksika ambayo huhusika katika kuunda neno kubalifu kileksika na kanuni ya kirai ambayo hutenda kazi baada ya neno kuundwa. Kihore na wezake (2003) wanaeleza, kuna uwezekano wa kuzalisha vitenzi kutoka katika katagoria

moja kwenda nyingine kwa mfano kivumishi < chafu> kinaweza kuwa kitenzi kwa kuingizwa kiambishi tamati <a> na kuwa <chafua>

4. 4.7 Utenzishwaji kutoka kategoria kutumia Iza, Ka, a, Ku

Utafiti umebaini kuwa muundo wa viambishi vinavyofanya kazi ya kubadili kategoria nyingine za maneno kuwa vitenzi umetumia kanuni ya ubainishaji wa viambishi, ambapo athari za kifonolojia zilizobainika zimezingatiwa, Athari iliyojitokeza ni ile ya udondoshaji kwa baadhi ya maneno na unyumbuaji kwenye maneno mengine. Baadhi ya maneno yaliyobainika kuchukua sifa hizo ni vivumishi, nomino na vielezi. Jumla ya asilimia 10.2 ya maneno yote yamejidhihisha katikamuundo huu na mifano yake ni kama inavyooneshwa kwenye jdwali Na.4.10.

Jedwali Na. 20 : miundo ya utezishaji kwa kutumia Iza, Ka, a, Ku

Kiambishi kitezishi	Aina ya neno kwa kategoria asili	Mtindo wa utenzishaji
Iza	Hima (E)	Himiza
Ka	Pevu (V)	Pevuka
A	Chafu (V)	Chafua
Ku	Tunu (N)	Tunuku

Utokeaji wa viambishi vilivyobadili kategoria moja na nyingine umebainika ila haikushughulikiwa sana kwa kutazama mabadiliko ya kategoria kama ndio lengo la msingi la kazi hii. Hata hivyo, ufafanuzi huu umetazama nadharia ya usarufishaji kwa namna inavyokubali kufanya kazi. Kwani, usarufishaji ni nadharia inayohusika na asili na mabadiliko ya maumbo ya kisarufi na tungo mbalimbali (Heine & Kuteva, 2005). Lengo la msingi la Nadharia ya Usarufishaji ni kufafanua namna maumbo ya

kisarufi na tungo mbalimbali yanavyojitokeza na kubadilika kwa kipindi fulani pamoja na kueleza kwanini yameundwa kwa namna yalivyo (Heine na Kuteva, 2005).

4.5 Mustasari wa Sura

Sura hii imefafanua uchambuzi wa data kwa kuzingatia malengo ya utafiti ambapo imebainishwa maneno yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Aidha, miundo iliyotumika kunominisha au kutenzisha imefafanuliwa kwa uwazi.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa tasnifu. Sura ina sehemu nne. Sehemu ya kwanza inazungumzia juu ya muhtasari wa tasnifu. Sehemu ya pili ni utoshelevu wa nadharia. Sehemu ya tatu inahusu mchango mpya wa utafiti huu. Na sehemu ya nne ni maoni na mapendekezo.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Kwa ujumla, tasnifu hii ilichunguza miundo inayotumika kunominisha na kutenzisha katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Ili kufikia malengo ya utafiti huu utafiti umebainisha maneno yanayonominishwa na kutenzishwa katika gazeti la *Zanzibar Leo*, sambamba na kuchunguza miundo mbalimbali inayotumiwa kutenzisha na kunominisha inayojidhihirisha katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Tasnifu hii, imegawiwa katika sura tano.

Utafiti ulianza kwa usuli wa mada, tamko la utafiti, lililofuatiwa na malengo ya utafiti. Sura hiyo pia imebainisha maswali, umuhimu na mipaka ya utafiti pamoja na nadharia zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data.

Sura ya Pili ni mapitio ya maandiko. Mtafiti alipitia vitabu, majarida, na hata baadhi ya tovuti, zilizomuwezesha kupata maelezo yanayohitajika kuhusiana na mada ya utafiti. Maelezo yalioelezwa katika sura hii yanahusu unominishaji na utenzishaji katika maeneo tofauti ya kitaaluma na baadaye kuhusisha na miundo inayotumika katika magazeti mbambali duniani. Katika maelezo hayo yamefafanuliwa mawazo ya

wataalamu kuhusu rejista za magazetini, uandishi wa magazetini duniani, uandishi wa magazetini Afrika na uandishi wa magazetini Tanzania. Vilevile, uundaji wa maneno kwa kutumia kategoria mbalimbali, Mwisho wa sehemu hiyo imeoneshwa pengo ya kiutafiti yaliyojitokeza kutokana na mapitio hayo.

Utafiti huu umeweka bayana mbinu na njia mbali mbali zilizotumiwa katika utafiti huu. Vile vile sura imeeleza eneo na mawanda ya utafiti, na pia jamii ya watafitiwa. Sura hii imeonesha pia juu ya umakinifu wa mbinu na vifaa vilivyotumika katika ukusanyaji wa data.

Pia, utafiti umeonesha namna data hizo zilivyochambuliwa na kutafsiriwa. Data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kifafanuzi. Uchambuzi uliongozwa na malengo ya utafiti pamoja na maswali yake kama yalivyooneshwa katika sura ya kwanza. Kutokana na malengo na maswali hayo, mtafiti alipata nafasi ya kutumia maswali yaliyokuwemo katika mbinu za udurusu wa maktabani. Kwa ujumla uchambuzi huo ulifanikiwa kwa vile uliweza kutoa matokeo yaliolingana na mabunio ya utafiti huu.

Kuhusu uchambuzi wa data utafiti ulikusanya jumla ya maneno takribani hamsini na moja na kuyachunguza namna yanavyotumika katika gazeti kwa miundo ya unominishaji na utenzishaji. Jumla ya maneno ishirini na sita yalibainika kuwa yametenzishwa kwa miundo mbalimbali na maneno hamsini na moja kunominishwa kwa miundo mbalimbali ya utenzishaji. Kwa hivyo. Kwa mujibu wa utafiti huu ni wazi kuwa gazeti *la Zanzibar Leo* linauwiano wa kunominisha na kutenzisha,

Utafiti huu pia, unawasilisha muhtasari wa tasnifu ya utafiti, utoshelevu wa nadharia zilizotumika katika utafiti, mchango mpya wa utafiti pamoja na maoni na mapendekezo yaliotokana na utafiti yanayopaswa kufanyiwa kazi kwa siku zijazo au katika tafiti zijazo.

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Jumla ya maneno hamsini na moja 51 yalichunguzwa utokeaji wake gazeti la Zanzibar katika miundo ya unominishi na utenzishaji. Maneno ishirini na nne 25 yaligunguliwa kuwa na miundo tofauti ya unominishaji ambayo yalichukua asilimia 47 katika jumla ya maneno yote. Maneno ishirini na saba 26 yalionekana kutenzishwa kwa miundo tofauti ambayo yalikuwa na asimilia 53 ya jumla ya maneno yote yaliyotenzishwa. Kwa ujumla miundo ya utenzishaji umejitokeza zaidi kwa mpishano wa asilimia 06 katika jumla ya maneno yote yaliyotafitiwa. Hivyo, tumeweza kubaini kuwa katika jamii lugha yeyote inaweza kuwa na miundo maalumu inayotumika katika uga wa kitaaluma au wa kijamii. Hivyo utafiti huu ni muhimu kwani umegundua mambo kadhaa ambayo yalikuwa hayajatafitiwa hasa kutoka katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

5.4 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika Kwenye Utafiti

Kutokana na misingi ya nadharia ya Mofolojia Leksika na nadharia ya usarufishaji mtafiti aliweza kufafanua maneno yaliyotezishwa na kunominishwa katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Nadharia ya usarufishaji ile ya Mofolojia Leksika ni nadharia faafu zaidi katika kuchambua miundo tofauti iliyotumika kutenzisha na kunominisha katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Kwa mujibu wa nadharia hizo uchambuzi wa data kulifanikiwa sana kwani misingi ya nadharia inakubali miundo ya ubadilishaji wa

viambishi unaoweza kubadilisha kategoria moja au nyengine, vilevile, mtafiti alibaini mchakato wa kuunda maneno unavyoweza kutumiwa katika shughuli za kila siku kwani nadharia hii inakubaliana na hali hiyo. Aidha kanuni zinazofungamana na zile zinazoachana kifomula zinakubalika katika nadharia hii ilhali upachikaji wa viambishi umudu kuzalisha kategoria nyingine ya neno. Mbali na kuzingatia misingi hiyo, mtafiti pia alikwenda sambamba na hatua zilizopendekezwa katika kuifanyia kazi nadharia hii ya Mofolojia leksika. Hivyo, alianza kuuchunguza masharti na miundo ya upachikaji wa maneno katika mizizi ya maneno na kubadili kategoria moja kwenda nyingine ambayo ndio msingi mkuu wa nadharia ya utafiti huu

5.5 Mchango Mpya wa Utafiti

Utafiti huu umebaini kuwa katika lugha kuna kanuni maalumu zinazoongoza uundaji wa maneno kutoka kategoria moja kwenda nyingine. Pia, utafiti umebaini miundo mengine inakwepa urazini hasa miundo inayotumika katika uandishi wa magazetini utafiti umebaini kuwepo kwa kanuni au masharti zuizi yanayokwepa katika kuunda maneno. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa yapo maneno yanayoundwa bila kufata kanuni mahususi za lugha na baadhi ya wakati kuchusha au kuwakera watumiaji wa lugha. Kwa mfano, neno habarisha linaonekana kuwakera mno watumiaji wa lugha hii ilibainikana kuwa katika lugha yapo makundi ya kiitifaki na kihafidhina yanayoshikilia misimamo mikali dhidi ya uundaji na uingizaji wa kategoria za maneno. Vilevile, utafiti umebaini kuwa matendo yote kanuni katika usarufishaji katika uandishi wa magazeti hutokea kwa unasibu na sio kwa utaalumu au kufuatwa kwa kanuni za lugha.

5.6 Hitimisho

Utafiti huu ulikuwa na dhumuni la kutathimini unominishaji na utenzishaji wa maneno ya Kiswahili katika rejista za magazetini. Lengo hili liliongozwa na malengo mahususi mawili ambayo ni Kubaini maneno yaliyonominishwa na yaliyotenzishwa katika lugha ya Kiswahili katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo* na kutathimini miundo inayotumika katika kunominisha na kutezisha katika habari za kawaida na habari za michezo katika gazeti la *Zanzibar Leo*. Lengo la kubainisha maneno yaliyotenzishwa na kunaominishwa lilifikiwa kwa kukusanya maneno hamsini na moja 51 ambayo yamenomishwa na yaliyotenzishwa. Maneno ishirini na tano 25 yaligunduliwa kuwa na miundo tofauti ya unominishaji ambayo yalichukua asilimia 47 katika jumla ya maneno yote. Maneno ishirini na saba 26 yalionekana kutezishwa kwa miundo tofauti ambayo yalikuwa na asilimia 53 ya jumla ya maneno yote yaliyotenzishwa. Lengo la pili lilichunguza miundo ya unominishaji na utenzishaji. Katika kuchunguza miundo hiyo, utafiti umebaini miundo ya utenzishaji imejitokeza zaidi kwa mpishano wa asilimia 06 katika jumla ya maneno yote yaliyotafitiwa. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha miundo mitano 05 ya unominishaji na miundo saba ya utenzishaji katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

5.7 Mapendekezo ya Utafiti

Mapendekezo yatokanayo na utafiti huu yamegawanyika katika makundi matatu makuu. Mosi, mapendekezo kwa waandishi wa magazetini. Pili, mapendekezo kwa, mapendekezo kwa serikali na tatu watafiti wajao.

5.7.1 Mapendekezo kwa Waandishi wa Magazeti

Waandishi wa magazeti wanapaswa kuwa na taaluma ya lugha ya Kiswahili kwa kujifundisha kanuni mbalimbali za uandishi na utumiaji wa lugha kwa ufasahaⁱ. Aidha, waandishi wanapaswa kufuatilia sarufi la lugha ya Kiswahili ili kuandika kwa uweledi zaidi. Pia, wahariri wa magazeti wanapaswa kuwa watu wenye taaluma ya uandishi pamoja na lugha ya Kiswahili.

5.7.2 Mapendekezo Kwa Serikali

Serikali ina jukumu kubwa la kuanzisha vyo vya uandishi wa habari ambavyo vitajiegemeza katika matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. pia, serikali ndio yenye jukumu la msingi la kukemea na kudhibiti matumizi mabaya ya maneno katika uandishi wa magazeti na kujiepusha na makosa ya sarufi na msamiati wa lugha .

5.7.3 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye

Utafiti huu ulitazama miundo ya unominishaji na utenzishaji katika rejista ya magazeti kwa kudurusu gazeti la *Zanzibar Leo* tu, jambo ambalo linatoa mwanya kwa watafiti wengine kutazama miundo tofauti ya uandishi pamoja na sarufi ya lugha.

Aidha, watafiti wanaweza kuchunguza mtiririko wa tungo unavyojitokeza katika gazeti hili. Pia watafiti wanaweza kutazama makossa ya uakifishaji yanavyojidhihirisha katika gazeti la *Zanzibar Leo*.

MAREJELEO

- Agu, I. E. (2015). *Linguistic-Stylistic Analysis of Newspaper Reportage*. Department of English and Literary Studies, Federal University Wukari-Nigeria
- Amadi, E. C. & Agava, L (2010). *Impact of Students failure in English Language and the Nigerian formal education in GOKANA*. Local government area of rivers state, Nigeria.
- Brown, H. D. (2000). *Principles of language learning and teaching* (4th edition). NY: Longman.
- Buberwa, A (2017). “*Ruwaza za Ki Mofolojia Za Majina Ya Mahali Ya Kihaya: Mtazamo Wa Mofolojia Leksika.*” Tasnifu Iliyowasilisha Kukamilisha Masharti ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar es Salamu. Haijachapishwa.
- Crystal,D na Davy,D (1969). *Investigating English style*. Longman group Publisher. Hong Kong.
- Dzahene-Quarshie, J. (2013). *Language Choice in Swahili Newspaper Advertising in Tanzania*. Ghana University Press. Legon, Accra-Ghana.
- Finnegan, R., (1978). *Oral Literature in Africa*. Oxford University Press. Nairobi.
- Gomov, M. (2012). “*On Stylistic Trends in Modern Swahili Poetry*”. *Style in Africa Literature*. Amsterdam-New York. Rodopi, 235-252
- Gupta, R. (2007). “*Bilingual advertising in a multilingual country*”. *Language in India*, 7, 1-14. *Important Information for Customars of DAWASCO*”

(Taarifa Muhimu kwa Wateja wa DAWASCO). (2006, January 20).
Mtanzania, p. 1

Habwe na Karanja (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*: Nairobi. Phonex
Publisher.

Hakimu, J. (2020). “*Ubantuishaji wa ki Mofolojia katika vitenzi vya Kiswahili
vyenye asili ya Kiarabu*” (Tasnifu ya uzamivu). Chuo Kikuu cha
Dodoma, Tanzania.

Hanifa (2008). *Prentice Prefix Used On Headline of Jakarta Post Newspaper*.
Indonesia Press.

Hansen na Drobnjakovic(2010). *Morphological Theory*. SAGE Publisher.

Heina na Kuteva (2005). *Language Contact and grammatical change*. Cambridge
University Press.

Hickey, R (2010). *The hand book of language contact*. Cambridge Univesity Press

Hopper, P. J na Traugott(2003). *Gramaticalization*: Cambrige Univesity Press.
London.

Kabellow J. K (2019). *Language Registers and their Influence in the Instruction of
English Language in Secondary School in Kenya*. Alupe University
College.

Katamba, F. (1993). *Morphology*: Macmillan.

- Kelly-Holmes, H. (2005). *Advertising as multilingual communication*. UK: Palgrave Macmillan.
- Kezilahabi, Euphrase. (1983). *Uchunguzi katika ushairi wa Kiswahili. Makala za semina ya kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*, Dar es salaam. TUKI.
- Kiango, J. G. (2000) *Bantu Lexicography: A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary Entries*. Tokyo. ILCAA.
- Kiango, J. G. (2007). *Kamusi ya Shule za Msingi*. Oxford University Press. Nairobi.
- Kihore, Y. M na wezake (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu*. Tasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dares Salam.
- King'ei (2000). *Matatizo Ya Matumizi Ya Lugha Katika Magazeti*. Swahili Forum.
- Kiparsky, P. (1982). *From cyclic phonology to lexical phonology*. In van der Hulst, Harry & Smith, Norval (eds.) *The structure of phonological representations*. Vol. 1. Dordrecht: Foris. 131–175.
- Kipury, N. (2002). *Oral Literature of the Masai*. Dar es Salaam: Ujuzi Educational Publishers.
- Kirichia, J. K. (2012). *Usawiri wa waniasia kama kuwahusisha katika makala za habari kwenye gazeti la Taifa Leo nchini Kenya*. Kenyatta University. Nairobi.

- Kombo, D. & Tromp, L. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Nairobi: Pauline Publications, Africa.
- Kothari, C. R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi India, Wiley Eastern.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology. Methods and Techniques Revised 2nd Edition*. New –Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.
- Laminory, B, De mulder, W na Carlier A (2012). *Introduction: the pace of gramaticalization*, Univesity of leuven.
- Lehman, P. R (2002). *A personal perspective*: SAGE Publishing.
- Lehmann, C. (1985) *Grammaticalization: Synchronic Variation and diachronic change*. *Lingua e Stile* 20, 303-318
- Lieber, R. L. (1990). *Statitistical Significance and Statistical Power in Hypothesis Testing*. Katika jarida la orthopaedic research. [https// doi.org/10.1002/jor](https://doi.org/10.1002/jor).
- Lusekelo, A (2010). *Morphology-Pragmatics Interface: The Case of the Tanzanian Commercials in Swahili Newspapers* (Dar es Salaam University College of Education/University of Botswana)
- Malangwa, P. S. (2011). *English Feature in Kiswahili Social media*. University of Dar es salam. Vol. 14, Na.1.
- Malgwi, G. J. (2009). *Increase Your Word Power: A Course in Vocabulary Development for Schools and Colleges*, Yola: Paraclete

- Masebo, M. na Nyangwine, N. (2012). *Kiswahili Kidato cha 3&4*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Massamba, D. P. B na wenzake (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Massamba na wenzake, (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. TUKI. Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B. (2010). *Phonological Theory; History and development*. TUKI. Dar es salaam.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Serengeti Educational Publisher
- Mberi, E. N. (2002). *The categorical status and functions of Auxiries in shona: A Dissertation Submitted To The Department Of African Languages And Literature Of The University Of Zimbambwe In Partial Fulfilment Of The Requirements For The Degree Of Doctor Of Philosophy*
- McMahou (2000). *Change, Chance and Optimality*. Oxford University Press.
- Meillet, A. (1912). *L'évolution des formes grammaticales*. Scienta (Rivista di Scienza) 12, No. 26,6.
- Mgullu, R. S. (2012) *Mtala wa Isimu: Fonetiki, Fonoloji Na Mofolojia ya Kiswahili*, Longhorn Publishers, Dare es salam, Tanzania.

- Mochiwa, Z. S. M. (2007): *Kiswahili Verb: A lexicographic challenge: AFRILEX-SERIES 17: 2007* kur. 114-133. <http://lexikos.journal.ac.za>.
- Mwansoko (1991). *Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam University Press. Dares Salam, Tanzania.
- Mwaro, A. G. (200). *Usayansi wa Isitilah za Isimu Ya Kiswahili*. Idara ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Mwijage, L. E. W. (2013) *Mimi ni sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo*. Prompt Printers and Publishers, Arusha, Tanzania.
- Ohly, Rajmund. (1987). *The Destabilization of the Herero Language* . (African studies of the Academy,2). Windhoek University of Namibia.
- Ponera, A. S (2019). *Misingi Ya Utafiti Wa Kitaamuli Na Uandishi wa Tasnifu*. Central Tanganyika Press, Dodoma, Tanzania.
- Saussure, F. de (1959). *Course in General Linguistics*. Paris: Philosophical Library.
- Schiffman, L. G, Hnsen, H na Kanuk, L. (2011). *Consumer Behavior: A European outlook*. Financial time prentice hall, New York.
- Shampungu (2019) *Ruwaza ya Kitenzi cha Kiswahili Mtazamo wa Mofolojia Leksika*. Tasnifu iliyowasilishwa kukamilisha shahada ya uzamili, Jomokenyata University, Kenya. Haijachapishwa
- Sperber, D, and Wilson, D. (1995). *Relevance: Communication and Cognition*. Oxford: Blackwell.

Stonham, J na Katamba, f (2006). *Morphology*. Palgrave. Macmilan.

Temu, C. W. (1981). "*Uundaji wa Maneno Mapya ya Kiswahili - Kichocheo cha Mjadala*, 1' Makala Yaliyosoniwa katika Kongamano la Kimataifa la Kiswahili (K. K. A.), Nairobi, Septemba 1981.

Traugott, E. C. and Heine, B. eds. (1991) *Approaches to Grammaticalization Volumes 1, 2*. John Benjamins Publishing Co., Amsterdam.

Waihiga. G (2011). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Sasa sema Publications, Nairobi, Kenya.

Wallace, R. A na Wolf, A. (1987), *Contemporary Sociologic Theory*. New York.

Yule, G. (2010). *The Study of Language* (4th edition). New York: Cambridge University Press

KIAMBATANISHO Na. 1

Msamiati wa msingi uliochunguzwa katika gazeti la Zanzibar leo kwa namna unavyoweza kunominishwa na kutenzishwa.

	NENO ASILI
1.	Aibu
2.	Andika
3.	Baka
4.	Bora
5.	Chachu
6.	Chafu
7.	Chagua
8.	Chekecha
9.	Cheza
10.	Chochea
11.	Choko
12.	Chuja
13.	Duni
14.	Elimu
15.	Fupi
16.	Fyeka
17.	Habari
18.	Hima
19.	Imba
20.	Jenga
21.	Jumla
22.	Kaa
23.	Kaanga
24.	Komboa
25.	Laini
26.	Laini

27.	Legea
28.	Lia
29.	Mbaya
30.	Omba
31.	Pamba
32.	Pekua
33.	Pembua
34.	Piga
35.	Pumu
36.	Rasmi
37.	Safi
38.	Taifa
39.	Tamka
40.	Tenda
41.	Tobo
42.	Tulia
43.	Ubepari
44.	Ujinga
45.	Uma
46.	Umba
47.	Vumilia
48.	Zawadi
49.	Zee
50.	Zembe
51.	Zuzu

Kiambatanisho Na 2

Mbinu ya maktaba

Kothari (2004) anaieleza mbinu hii kuwa ni mbinu inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo.

Ewan na Calvet(2004) wanaelezakuwa maktabani ni mahali palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida, na magazeti kwa wasomaji na watafitiwa kada tofauti za taaluma.

Mbinu hii ya maktabani itamsaidia mtafiti huweza kupata data kwa kupitia mapitio mbali mbali kwani mtafiti atasoma vitabu, makala na magazeti ya Zanzibar Leo ambayo huhusiana na mada ya utafiti. Hapo ndipo mtafiti atafahamu kilichoandikwa na watafiti waliotangulia juu ya mada husika kisha kuweza kubaini pengo lililopo katika mada inayofanyiwa utafiti

Kiambatanisho namba 03



Neno tangazo ambalo ni nomino limetanzishwa kwa kuambikwa kiambishi awali {ku} ya utezishi na kupachikwa irabu ya kauli.





Neno ahadi ambalo ni nomino limetenzishwa kwa kuingiza kiambishi {A}nafsi ya utendaji na kubadilika kuwa kitenzi



Neno “zoa” ambalo ni kitenzi limenominishwa na kuwa “mazoezi”ambalo ni nomino.

ZANZIBAR

Tembelea :- www.zanzibarleo.co.tz

[Zanzibarleo](#)
[Zanzibarleo](#)
[Zanzibarleo](#)
[Zanzibarleo](#)

Jamata 35 Agosti 2021. **KWA UKWELI NA UWAZI** ISSN 1821-8599 Ileo NO.6313. **LEO** TSH. 500/=

Hemed: Viongozi CCM sikilizeni wananchi

Uhakiki wanachama Masterlife kuanza leo

HABARI UK. 3



MALUMBIU wa Kwanza Kuu ya Mafananchani Kuu ya CCM TSH. Wazazi Zafwanzi Abubala, ukumbukaji/kuji kwa ya kwanza wa CCM zinao ya wakikwa wa maendeleo ya shulizi wakati uliopo/kuji kwa maendeleo hayo wakati pando za Mafananchani, wakazi wa Kuu ya Uvuzi. (MCOA NA CCM)

<p>SMZ kuendeleza ushirikiano na Pakistani HABARI UK. 3</p>	<p>SMZ, SMT zajidhatiti kuimarisha msaada wa sheria HABARI UK. 3</p>	<p>Wazazi wahimizwa kufuatilia maendeleo ya wanafunzi HABARI UK. 15</p>
---	--	---

Neno “shirika” ni nomino limeambishwa kiambishi awali cha utenzishi {u} na kupachikwa irabu {o} kama kiambishi tamati maana.